epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US
Ijumaa Machi 29, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0581630
www.ippmedia.com
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital



**ACT** na hoja 10 mkononi Uchaguzi wa Serikali za Mitaa 2024

UKURASA 4

**Adaiwa** kujiua kwa sumu akiwa kituo cha polisi

UKURASA 7



**CHADEMA** yajipanga kuendeleza maandamano

UKURASA 9




UKURASA 22

**NITASTAAFU NISIPOWEZA KUISAIDIA TIMU - MESSI**

## RIPOTI ZA CAG, TAKUKURU

# Ulaji ulivyo

UKURASA 3



Rais Samia Suluhu Hassan akipokea Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa Mwaka 2022/23 kutoka kwa CAG Charles Kichere, Ikulu Chamwino, mkoani Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

### TAKUKURU

1. **Safari hewa zaondoka na bilioni 1.3/-**
2. **Bil. 12/- zayeyuka Jiji la Dar, DART; hoteli zashikiliwa**
3. **Harufu ya rushwa ujenzi wa vituo vipya vya mafuta**
4. **Kampuni za simu zapotosha bilioni 76/-**
5. **Bilioni 87/- zaokolewa, kesi mpya 600 kortini**

### HOJA ZA CAG

1. **Hati safi zapaa, TTCL na TRC zapunguza hasara**
2. **Zabuni tata MSD, TANESCO, serikali ilipe bil. 208/- NHIF**
3. **Kilio mabilioni ya Bwawa la Nyerere**
4. **Baadhi mashirika ya umma bado ngome za hasara**
5. **CAG kukagua The Hague, AU na EAC**

**MICHEZO** SIMBA SC, AL AHLY NI ZAIDI YA VITA UK.24 **KATUNI** UK.6

## RIPOTI YA CAG 2022/23

# Yaanika ulaji ulivyo

RIPOTI ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka 2022/23 imekabidhiwa kwa Rais, ikiibua ulaji wa fedha za umma, huku utendaji katika baadhi ya taasisi ukiimarika.

Akikabidhi ripoti hiyo kwa Rais Ikulu, Chamwino, mkoani Dodoma jana, CAG Charles Kichere, alibainisha kuwa kwa mwaka huo wa ukaguzi, ofisi yake imetoa hati 1,209 za ukaguzi. Kati yake, hati safi ni 1,197 sawa na asilimia 99, hati zenye shaka ni tisa, hati mbaya ni moja na hati mbili za kushindwa kutoa maoni.

CAG alisema kuwa hadi Juni 30, 2023, Deni la Serikali lilikuwa Sh. trilioni 82.25 sawa na ongezeko la asilimia 15 kutoka Sh. trilioni 71.31 kwa 2021/22.

"Deni hilo linajumuisha Deni la Ndani Sh. trilioni 28.92 na la nje Sh. trilioni 53.32. Kipimo cha Deni la Serikali kinachotumia Pato la Taifa kinaonesha deni hili ni himilivu,"alisema.

CAG alifafanua kuwa uwiano wa kulipa madeni na mauzo ya nje ni asilimia 12.7, chini kidogo ya kiwango cha ukomo cha asilimia 15 na uwiano wa malipo ya madeni na mapato ni asilimia 14.3, chini ya kidogo ya kiwango elekezi cha asilimia 18.

Vilevile, alisema ukaguzi katika Mamlaka ya Mapato (TRA) umebaini makusanyo ya kodi Sh. trilioni 22.58 kwa mwaka 2022/23 sawa na ongezeko la asilimia nane kulinganishwa na Sh. trilioni 20.94 mwaka 2021/22.

"Licha ya ongezeko hilo, makusanyo hayo yalikuwa chini Sh. trilioni 1.07 sawa na asilimia 4.5 ya makadirio," alisema na kubainisha kuwa alibaini TRA inakabiliwa na tatizo la udhibiti wa bidhaa zinazopita nchini kuelekea nchi jirani kutokana na upungufu wa ving'amuzi vya kielektroniki ambao unadhoofisha ufanisi katika kuhakiki mizigo inayokwenda nje ya nchi.

Pia alibaini upungufu katika utoaji mizigo inayotokana na ving'amuzi kukosekana kwenye mfumo wa ECTS, kuwa na taarifa zisizo sahihi na kutowiana kwa taarifa kati ya vifaa saidizi na vifaa vikuu kwenye mfumo.

Kuhusu mapato yasiyo ya kodi, CAG alisema amebaini mashirika manane ya umma yalikusanya mapato ya Sh. bilioni 23.27 nje ya mfumo wa kielektroniki wa malipo ya serikali (GEPG), hivyo kukiuka Waraka wa Hazina Na. 3 wa Mwaka 2017.

**MADUDU H'SHAURI**

CAG alisema kuna mapato yasiyokusanywa ya Sh. bilioni 61.15 na mapato yasiyowasilishwa benki ya Sh. bilioni 6.19 kutoka vyanzo muhimu na vikubwa kwenye halmashauri, hali inayoathiri uwezo wa mamlaka za serikali za mitaa kutekeleza miradi na kutoa huduma bora kwa jamii.

Alisema mamlaka 184 za serikali za mitaa hazikutenga Sh. bilioni 20.23 za mapato ya ndani kwa ajili ya miradi ya maendeleo na shughuli za uendeshaji vijiji au mitaa.

Pia alisema uchunguzi umebaini kuwapo halmashauri 10 zilizolipa jumla ya Sh. bilioni 2.95 kwa kazi zilizotekelezwa bila kuwapo nyaraka zinazoonyesha ukubwa wa kazi.

"Na mamlaka nne zililipa Sh. milioni 346.69 kwa kazi ambazo hazikutekelezwa kutokana na kutokuwapo usimamizi unaoridhisha wa miradi. Hii inakawamisha juhudi, uwazi na uwajibikaji katika mchakato wa malipo hasa kwenye utekelezaji miradi ya maendeleo," alisema.

**DOSARI MSD**

CAG pia alisema ukaguzi umebaini Bohari ya Dawa (MSD) imetoa zabuni ya vifaa vya maabara vya upimaji wa Uviko-19 na kubaini kampuni iliyopewa kazi hiyo haikuwa mtengenezaji wa vifaa hivyo kinyume cha masharti ya zabuni.

"Baada ya vifaa kufika, wataalamu walibaini havifai kwa mashine zetu na MSD ililipa fedha zote. Ninapendekeza hatua zichukuliwe kwa wahusika na kurejesha fedha hizo za umma," alisema.

CAG Kichere pia alisema amebaini utaratibu duni katika utekelezaji miradi, akifafanua: "Taasisi kama TANESCO na taasisi za huduma za maji zinaingilia barabara zinazosimamiwa na TARURA. Kwa mfano, Arusha serikali ilitumia Sh. bilioni 194.53 katika mradi wa barabara lakini ukaharibiwa na kazi za mamlaka ya maji ambayo ilianza tu baada ya barabara kukamilika, hivyo wanatakiwa kuingia gharama nyingine kwa kuharibu miundombinu."

**MITA TANESCO**

CAG alisema ukaguzi wake katika mita za umeme umebaini mita 108,088 kati ya 602,266 zilibadilishwa na TANESCO kabla ya kipindi cha uhai wa matumizi yake kuisha. Kati yake, mita 13,493 zilibadilishwa ndani ya mwaka mmoja baada ya kufungwa kwake.

"Na mita 94,595 zilikuwa na muda mfupi wa matumizi kati ya mwaka mmoja hadi 15 kinyume cha muda unaokubalika wa miaka 20 kwa mujibu wa TANESCO wenyewe," alisema na kutoa angalizo kuwa kubadilisha mita mapema kunasababisha gharama kubwa kwa shirika.

Pamoja na hayo, CAG alisema amebaini TANESCO kuchelewa kutekeleza miradi ya kijamii (CSR) yenye thamani ya Sh. bilioni 262 toka Mradi wa Kufua Umeme wa Bwawa la Nyerere (JNHPP).

"Katika mradi huu, CSR ilikuwa ni kujenga kituo cha michezo na kuboresha barabara. Hata hivyo, ilitokea hali ya kutoelewana kati ya TANESCO na mkandarasi na kusababisha mabadiliko kadhaa ikiwamo kujenga vituo vya ufundi kwenye maeneo mbalimbali na mabadiliko haya yamesababisha kuchelewa kwa makubaliano ya kina kuhusu utekelezaji miradi ya kijamii na kuhatarisha uwezo wa mradi wa kuwapa faida na



Rais Samia Suluhu Hassan

mradi wananchi," alisema.

**USIMAMIZI MIKATABA**

CAG pia alisema uchunguzi umebaini matumizi yasiyo na tija ya fedha za umma katika taasisi mbalimbali za serikali yanayosababisha hasara ya zaidi ya Sh. bilioni 222.34.

"Hasara hii inatokana na kucheleweshwa malipo kwa makanadarasi wenye miradi ya barabara na hivyo kusababisha malipo makubwa ya riba," alisema.

CAG pia alisema amebaini katika miradi ya barabara, meli, vivuko, maji na umeme kuna matatizo yanayoathiri utekelezaji wake ikiwamo kuchelewa kukamilika kwa miradi na mingine kukamilika kwa kiwango cha chini na kuongeza gharama za ukamilishaji.

"Tulichukua miradi mitano ya barabara zinazosimamiwa na TANROADS na tukagundua gharama zake ziliongezeka kwa Sh. bilioni 130, ukaguzi wa kiufundi wa udhibiti wa gharama umebaini kulikuwa na ongezeko la gharama Sh. bilioni 130.51 ambalo limesababishwa na upungufu mkubwa ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina usio sahihi umesababisha ongezeko la gharama Sh. bilioni 44.97 sawa na asilimia 34 ya gharama zote za ziada.

"Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (TPA) ilisitisha miradi ya miaka ya nyuma yenye thamani ya Sh. bilioni 26.68 kwa mwaka 2022/23 na ilitokana na tathmini iliyoonesha kwamba miradi hii haitekelezeki licha ya kulipiwa fedha na ilifutwa kama hasara," alisema na kueleza kuwa uamuzi huo umetokana na usimamizi duni wa miradi na upembuzi yakinifu usiokidhi haja.

**HASARA YAPUNGUA**

Alisema Shirika la Mawasiliano (TTCL) kwa mwaka 2022/23 limepata hasara ya Sh. milioni 894, ikipungua kwa asilimia 94 kulinganishwa na hasara ya Sh. bilioni 19.23 ya mwaka uliopita.

"Shirika limetengeneza hasara hii licha ya kupokea ruzuku ya Sh. bilioni 4.55 kutoka serikalini na kuonesha kiasi cha Sh. bilioni 4.4 ikiwa ni sehemu ya ruzuku hiyo kama mapato yake kwa mwaka 2022/23," alisema.

CAG alisema Shirika la Reli Tanzania (TRC) limepata hasara ya Sh. bilioni 100.7 ambayo imepungua kwa asilimia 47.32 kulinganishwa na hasara ya Sh. bilioni 190.01.

"Hasara hii imetokea licha ya kupokea ruzuku ya Sh. bilioni 32.81 kutoka serikalini kwa ajili ya matumizi ya kawaida,"alisema.

CAG alisema kampuni ya uwekezaji ya TANOIL ilipata hasara ya Sh. bilioni 76.56 ikiwa ni ongezeko la Sh. bilioni 68.72 kutoka hasara ya Sh. bilioni 7.84 kwa mwaka uliotangulia.

Alisema hasara ilitokana na mafuta kutoka nje kuzuiwa na TANOIL kushindwa kuwalipa wauzaji na gharama kubwa ya kuhifadhi mafuta Sh. bilioni 12.9 kulinganishwa na Sh. bilioni 6.1 ya mwaka uliotangulia.

Pia alisema mapato ya kampuni kutokana na mauzo ya mafuta yalipungua kwa Sh. bilioni 296 sawa na asilimia 49. Waliuza lita za mafuta milioni 112 kulinganishwa na lita milioni 264 kwa mwaka uliotangulia.

CAG alisema Shirika la Posta lilipata hasara ya Sh. bilioni 1.34 kulinganishwa na faida ya Sh. bilioni 16.21 kwa mwaka uliopita na faida hiyo ilitokana na mauzo ya mali za shirika si biashara.

**ANGALIZO**

CAG Kichere pia alitoa angalizo kwa serikali kuhusu kuunganisha mashirika yanayojiendesha kwa hasara na mengine kufutwa na kupendekeza zoezi hilo liwe shirikishi kwa taasisi zote muhimu za serikali ili kuhakikisha uwazi, uwajibikaji na ufanisi katika mchakato huo.

"Taasisi za kushirikishwa ni pamoja na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali, Mkurugenzi Msimamizi wa Mali za Serikali na Msajili wa Hazina. Ninatoa angalizo hili hasa linapokujia suala la kugawana mali na madeni ambapo huwa kuna changamoto,"alisema.

Alitolea mfano Sh. bilioni 2.6 zilizokuwa bakaa kutoka Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam iliyovunjwa hakijagawanywa hadi sasa tangu mwaka 2020/21.

"Hii inachangia kupotea kwa mali na fedha, ninaendelea kuangalia hizi fedha zipo wapi. Pia ninashauri Shirika la NDC kuangalia kwa umakini kutokana na unyeti wa mambo yake na serikali itoe mtaji wa taasisi kama hizi ili kuboresha utendaji wao," alishauri.

**CHETI KIMATAIFA**

CAG pia alisema kuwa Januri 6, mwaka huu, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi (NAOT) ilipata cheti cha kutambulika kimataifa kwa mfumo wa usimamizi wa ubora kilichotolewa na taasisi ya kimataifa ya viwango vya ubora.

"Ofisi yangu pia imeendelea kukagua Kamisheni ya Usimamaizi wa Anga la Afrika ambayo makao makuuu yake yako mjini Dakar, Senegali kwa mkataba wa miaka mitatu utakaokamilika 2025, tunaendelea na mkataba wa kukagua Umoja wa Afrika, mkataba utakaokamilika mwaka huu 2024," alisema.

CAG alisema kwa kushirikiana na nchi zingine wanachama, ofisi yake pia inakagua Jumuiya ya Afrika Mashariki na taasisi zake.

"Tumepata mkataba mwingine wa miaka sita wa kukagua mahakama maalum inayoshughulikia kesi za watu waliohusika na uhalifu wakati wa vita vya wenyewe kwa wenyewe nchini Sierra Leone. Mahakama hii iko The Hague, Uholanzi,"alisema.

**NHIF**

CAG pia alisema Mfuko wa Taifa Bima ya Afya (NHIF) umekuwa ukipata hasara kwa miaka mitano iliyopita na kwa mwaka 2022/23 hasara ilikuwa Sh. bilioni 156.77, ikipungua kutoka Sh. bilioni 205. 95; michango ya wanachama imeongezeka kwa asilimia 14.6 na matumizi yameongezeka kwa asilimia 10.

Alisema kuna mambo yanaweza kuathiri uhai wa muda mrefu wa mfuko ikiwamo mikopo ya serikali ambayo haijalipwa ya Sh. bilioni 208 inasababisha mzigo mkubwa wa kifedha na serikali kwa mwaka 2024/25 imepanga kulipa Sh. bilioni 180.

"Wastaafu na wenza wao kunufaika bila kuchangia kunagharimu mfuko Sh. bilioni 84.7 kwa mwaka, kuongezeka kwa magonjwa yasiyo ya kuambukiza pia kunagharimu mfuko Sh. bilioni 137.8 kwa mwaka, hizi ni changamoto zinazoongeza shaka ya uhimilivu wa mfuko. Ninapendekeza mfuko ufikirie mikakati ya kuzalisha faida na serikali ilipe mikopo yake,"alisema.

CAG pia alisema Benki ya Maendeleo ya TIB inakabiliwa na tatizo la utoshelevu wa mtaji ambapo hadi Desemba 2023 ilikuwa na Sh. bilioni 88.12 wakati masharti yanataka iwe na mtaji wa Sh. bilioni 200.

"Serikali inapanga kutoa mtaji wa Sh. bilioni 118, hatua hii ni muhimu sana lakini haitoshi kwa kuwa TIB inamdai Msajili wa Hazina Sh. bilioni 37 tangu 2019," alisema.

**MFUMO WA MISHAHARA**

CAG pia alisema amebaini tatizo kwenye Mfumo wa Pamoja wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara (HCMIS) ambao unaruhusu watumishi kupokea mishahara wakiwa likizo za bila malipo, kupandishwa vyeo bila kukidhi miaka mitatu ya utumishi, kushushwa vyeo bila mabadiliko ya mshahara na kuwapa watumishi wenye namba za utambulisho zinazofanana.

**AFYA YA AKILI**

Mdhibiti huyo pia alisema amebaini upatikanaji huduma ya afya ya akili una upungufu na kuathiri jamii; utambuzi wa wagonjwa haufanywi kwa ufanisi katika ngazi ya jamii.

Alisema utambuzi unaofanywa unalenga zaidi watumiaji dawa za kulevya, wazee, walemavu, watoto waliopata mimba na wanaoishi mazingira magumu na kupuuza wengine, hali inayotokana na upungufu wa wataalamu ngazi ya jamii kwenye vijiji na mitaa.

RIPOTI YA TAKUKURU 2022/23

# Yafumua wizi mabilioni ndani ya serikali

## -Jiji la Dar, DART zayeyusha bilioni 12/-
## -Harufu rushwa vituo vya mafuta mitaani

Na Romana Mallya

RIPOTI ya mwaka 2022/23 ya utendaji kazi wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) imeibua udhaifu kiutendaji na vitendo vya rushwa katika taasisi za serikali, baadhi ya vigogo wakifikishwa mahakamani na hata kuhukumiwa kifungo gerezani.

Miongoni mwa 'madudu' yaliyobainika, ni malipo ya fedha za utekelezaji miradi ilhali miradi yenyewe haijatekelezwa, ujenzi holela wa vituo vya mafuta na nyaraka feki kudhibitisha malipo ya safari za nje.

Akikabidhi ripoti hiyo kwa Rais Samia Suluhu Hassan, Ikulu, Chamwino, Dodoma jana, Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU, Kamishna Salum Hamduni, alitaja miradi iliyofuatiliwa ni pamoja na miradi ya maendeleo inayotekelezwa kwa utaratibu wa Force Account na miradi 12 ya ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji yenye thamani ya Sh. bilioni 107.4 katika mikoa ya Morogoro, Dodoma, Iringa, Tabora na Mbeya.

Alisema matokeo ya ufuatiliaji yalionesha kuwapo mianya ya rushwa, baadhi ya miradi ilionekana kutosajiliwa na Bodi ya Usajili ya Makandarasi na Wakala wa Usalama Mahali Pa Kazi na ucheleweshaji wa malipo kwa makandarasi.

"Matokeo mengine ni malipo kufanyika pasipo kufanyika baadhi ya kazi, malighafi za ujenzi kutopimwa ubora wake kinyume cha mkataba na kutozingatiwa kwa sheria na kanuni za ununuzi wa umma na kuwapo kwa nyongeza ya kazi pasipo kufuata utaratibu," alisema.



Rais Samia Suluhu Hassan akipokea Taarifa ya Utendaji Kazi wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kwa mwaka 2022/2023 kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi hiyo, CP Salum Hamduni, Ikulu Chamwino, mkoani Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

### HATUA TAKUKURU

Kamishna Hamduni alisema TAKUKURU ilichukua hatua ikiwamo kuhakikisha marekebisho kwenye miradi husika yanafanyika ili serikali isipate hasara, pia kutoa elimu na kushauri wasimamizi wa miradi na mamlaka husika namna bora ya kuziba mianya ya rushwa iliyobainika.

Alisema katika ufuatiliaji wa miradi 1,800, miradi 171 yenye thamani ya Sh. bilioni 143.3 ilibainika kuwa na utekelezaji hafifu na kuanzisha uchunguzi. Miradi hiyo ni ya sekta za ujenzi, fedha, maji, kilimo na majengo.

"Mapendekezo 3,668 yalitolewa ili kurekebisha kasoro zilizobainika katika ufuatiliaji huo kuhakikisha marekebisho kwenye miradi husika yanafanyika kwa fedha ya mkandarasi au fedha iliyofujwa inarejeshwa serikalini.

"Jumla ya mapendekezo 2,740 yalitekelezwa sawa na asilimia 89.4 ya utekelezaji mapendekezo yaliyotolewa na TAKUKURU.

"TAKUKURU ilifanya kazi 790 za uchambuzi wa mifumo ya utoaji huduma kwa lengo la kubaini mianya ya rushwa na kushauri namna ya kuziba.

"Kwa ujumla uchambuzi ulibaini baadhi ya watendaji waliokuwa wanasimamia miradi ya Force Account kutokuwa na uelewa au kuwa na uelewa mdogo kuhusu taratibu za ununuzi.

"Ukiukwaji sheria na miongozo wakati wa kuunda kamati za usimamizi, ukiukwaji sheria wakati wa kufanya ununuzi na usimamizi wa miradi, kutokuwapo mfumo wa uthibiti wa weledi na taaluma katika utekelezaji miradi inayotumia Force Account.

"Upungufu wa wataalam, ukosefu wa fedha za usimamizi na ufinyu wa muda wa utekelezaji miradi na kutokuwapo kwa ukomo wa matumizi ya njia ya Force Account," alisema.

Kamishna Hamduni alisema ili kuondokana na upungufu huo, TAKUKURU iliwasilisha mapendekezo Mamlaka ya Kudhibiti Ununuzi wa Umma (PPRA) na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

### VITUO MAFUTA

Bosi huyo wa TAKUKURU alisema taasisi hiyo pia ilifanya uchambuzi wa uzingatiwaji mfumo wa taratibu za ujenzi wa vituo vya mafuta katika mikoa ya Dar es Salaam na Pwani.

"Uchambuzi huu ulihusisha vituo vya mafuta 38. Asilimia 79 ya vituo vilivyofikiwa katika uchambuzi vilizingatia sheria kwa kuwa na vibali vya ujenzi kutoka katika halmashauri ambako uwekezaji umefanyika.

"Asilimia 21 ya vituo vilivyofikiwa havikuwa na leseni wakati ufuatiliaji unafanyika. Tulibaini kuwapo ongezeko la maombi ya ubadilishaji matumizi ya ardhi kutoka yaliyopangwa awali na kuwa vituo vya mafuta.

"Pia tulibaini tatizo la ujenzi wa vituo vya mafuta katikati ya makazi ya watu; vinaongezeka na kuleta hofu na usalama kwa wananchi. TAKUKURU imewasilisha mapendekezo namna ya kukabiliana na upungufu huo na kuwasilisha kwa mamlaka husika," alisema.

### RUSHWA MSITUNI

Kamishna Hamduni pia alisema walifanya tathmini ya hatari ya rushwa katika uvunaji na usafirishaji mazao ya misitu na yenye hatari ya rushwa ni kwenye uundwaji kanuni na miongozo ya uvunaji na usafirishaji mazao ya misitu, usimamizi wa uvunaji, usafirishaji, upatikanaji leseni na mfumo wa ukusanyaji kodi ukionekana kuwa na udhaifu.

Alisema katika kipindi cha mwaka 2022/23, kupitia operesheni mbalimbali za uchunguzi, TAKUKURU imeokoa Sh. bilioni 87.59, ikiwa ni pamoja na Dola milioni 33 (Sh. bilioni 76.34) kupitia uchunguzi wa Mkongo wa Taifa.

Katika hilo, Kamishna Hamduni alisema ilibainika Umoja wa Watoa Huduma za Mawasiliano ulijenga miundombinu ya mawasilinao kinyume cha makubaliano na kuikosesha serikali mapato kutokana na huduma zao kutopita katika Mkongo wa Taifa.

"Kupitia mkataba wa makubaliano katika ya Umoja wa Watoa Huduma za Mawasiliano na Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia, umoja huo ulikubali kulipa Dola milioni 20 katika kipindi cha miaka mitano na kulipa pamoja na riba ya asilimia 3.5 kwa mwaka na Dola milioni 13 zitalipwa kwa njia ya uwekezaji kati ya serikali kupitia wizara husika," alisema.

Uokoaji mwingine aliutaja ni wa Dola milioni 2.971 (Sh. bilioni saba) zilizotokana na mkataba ulioingiwa mwaka 2007 kati ya Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na Pangea Minerals Limited.

Alisema pia wameokoa Sh. bilioni nne za halmashauri zilizochepushwa na kupitia uchunguzi, zilirejeshwa katika halmashauri na sekretarieti za mikoa.

"Vyama vya ushirika tumedhibiti na uokoaji fedha milioni 248.8 zilizofanyiwa ubadhirifu, zilirejeshwa katika vyama.

"TAKUKURU pia imechunguza na kukamilisha majalada 900 yakiwamo 21 ya rushwa kubwa, yakihusisha ubadhirifu na hasara kwa serikali ikiwamo wa Sh. bilioni 8.9 zilizokusanywa kwa njia ya mashine za POSS na Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam.

"Fedha hizi hazikupelekwa benki, lakini watuhumiwa walighushi nyaraka wakionesha zimepelekwa benki. Uchunguzi wa ubadhirifu wa Sh. bilioni nne zilizotokana na makusanyo ya TANAPA, Mamlaka ya Uhifadhi ya Eneo la Ngorongoro (NCAA) na Bodi ya Utalii umefanyika," alisema.

### SAFARI HEWA

Kamishna Hamduni alisema uchunguzi mwingine ni wa safari hewa nje ya nchi zilizosababishia NCAA hasara ya Sh. bilioni 1.3 na uchunguzi wa upotevu wa Sh. bilioni 14 uliofanywa na iliyokuwa menejimenti ya DART.

"Uchunguzi kuhusu ukodishaji wa maghala ya UDA kinyume cha utaratibu na kuisababishia serikali hasara ya Sh. bilioni 20.5 umefanyika pamoja na upotevu wa vipuri vya UDART uliosababishia serikali hasara Sh. bilioni 3.29.

"Pia tumefanya uchunguzi wa Sh. bilioni nne uliohusu ukiukwaji wa taratibu za ununuzi katika Mamlaka ya Bandari ya Tanzania (TPA) kwenye Bandari ya Dar es Salaam wakati wa ununuzi wa mfumo wa Enterprises Resources Plan uliofanywa na kampuni ya Zimbabwe.

"TAKUKURU pia imefanya uchunguzi wa Sh. bilioni 1.6 zilizochepushwa na kufanyiwa ubadhirifu Bandari ya Kigoma ambako watuhumiwa walighushi saini wakishirikiana na watumishi wa benki na kufanikiwa kutoa fedha hizo," alisema.

### RIPOTI CAG

Kuhusu hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Kamishna Hamduni alisema walizipitia na kufungua majalada 375 yenye viashiria vya rushwa na jinai.

Alifafanua kuwa majalada 156 yalifungwa kwa kukosa ushahidi na jinai na majalada 73 walibaini watendaji wa serikali walikiuka taratibu, lakini hawakupata ushahidi wa jinai, bali wa kuwachukulia hatua za kinidhamu.

"Mashauri 114 yalifunguliwa mahakamani na 41 yaliamuliwa na kati ya hayo, mashauri 40 tulishinda na kupoteza shauri moja. Majalada 160 uchunguzi unaendelea," alisema.

Kamishna Hamduni alisema TAKUKURU pia ilifanyia kazi majalada yanayotokana na Kiongozi wa Kitaifa wa Mbio za Mwenge ambapo kwa mwaka jana miradi 20 ilikataliwa.

Kwa ujumla, katika mwaka huo, kesi mpya 600 zilifunguliwa mahakamani. Kati yake, 594 zilifunguliwa mahakama za chini na sita Mahakama Kuu Divisheni ya Rushwa na Uhujumu Uchumi. "TAKUKURU na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka inachunguza na kuweka zuio za mali zinazodhaniwa kupatikana kwa rushwa ambazo ni magari 15, mashamba sita, hoteli tatu, nyumba za kulala wageni nne, viwanja 29, nyumba za makazi 25, baa mbili, fremu mbili za maduka na shule moja," alisema.



Msemaji wa familia ya Waziri Mkuu wa zamani, Hayati Edward Sokoine, Lemburis Kivuyo akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dodoma jana, kuhusu kumbukizi ya miaka 40 ya kifo cha Sokoine, itakayofanyika Monduli Juu, mkoani Arusha Aprili 12 mwaka huu na mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Rais Samia Suluhu Hassan. **PICHA IBRAHIM JOSEPH**

# ACT: Yafanyike haya uchaguzi wa serikali mitaa 2024 uwe huru

**Na Sabato Kasika**

CHAMA cha ACT Wazalendo kimetaja mambo kinayoamini yakipewa kipaumbele yatasaidia kufanikisha uchaguzi wa serikali za mitaa unaotarajiwa kufanyika mwaka huu.

Ni baada ya kuwa kimepitia Sheria mpya ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi 2024 ambayo imetiwa saini na Rais na kuwa sheria na kuchapishwa kwenye Gazeti la Serikali Na. 12 la tarehe 22 Machi 2024.

Naibu Katibu wa Habari, Uenezi na Uhusiano na Umma, Shangwe Ayo, alitaja orodha ya mambo hayo jijini Dar es Salaam alipozungumza na waandishi wa habari.

Moja ya mambo hayo ni kutumika kwa Daftari la Tume ya Uchaguzi kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

Mbali hilo, Ayo alisema kuna haja kuwa na uwazi na ushirikishwaji wadau katika uzalishaji, uhifadhi na usambazaji karatasi za kupigia kura na nyaraka nyingine za uchaguzi.

"Sheria itamke bayana kuwa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi itawashirikisha wadau wa uchaguzi ikiwamo vyama vya siasa katika michakato yote inayohusu karatasi za kupigia kura," alisema.

Ayo alisema hatua hiyo itasaidia kuepuka kadhia ya karatasi hizo kutumika vibaya kutokana na uzoefu wa Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 na uchaguzi wa marudio ulioitishwa mara sita tangu mwaka 2021.

Katika orodha hiyo ya mapendekezo ya ACT Wazalendo, Ayo alisema mawakala wa vyama vya siasa wawe huru kwa kuwa ni wajibu wao kulinda maslahi ya wagombea na vyama vyao, pia utaratibu wa mawakala kula kiapo cha uaminifu uondolewe kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

"Wajibu wa kutambulisha na kubadilisha mawakala wa uchaguzi uachwe kwa vyama vya siasa na wagombea wenyewe. Pia, uhuru wa mawakala kwenye vituo vya kupigia kura uzingatiwe, ikiwamo haki ya kuingia na madaftari ya wapigakura na simu," alisema.

Katika pendekezo lingine, sheria iweke sharti kwa wasimamizi wa uchaguzi kubandika matokeo katika vituo vya uchaguzi na kugawa nakala ya fomu za matokeo kwa mawakala wa vyama vya siasa.

"Tume ichapishe nakala za kutosha za fomu za matokeo kuepusha visingizio vya kukosekana kwa nakala za fomu za matokeo ambavyo hutumika kuwanyima mawakala fomu hizo," alisema.

Katika pendekezo lingine, Ayo alisema chama hicho kinataka Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa ijikite katika sifa za msingi za kikatiba kwa wagombea kama vile uraia, umri, utimamu wa akili, kudhaminiwa na chama cha siasa na kujua kusoma na kuandika.

Mbali na hilo, alisema sifa ngumu kuthibitisha, ambazo zimekuwa zikitumika kuwaengua wagombea wengi wa upinzani kama vile kuwa na shughuli halali ya kumwingizia kipato zisijumuishwe kwenye sifa za kugombea na pia muda wa kampeni usipungue wiki mbili.

"Uzoefu wa uchaguzi uliopita wa serikali za mitaa 2019, kampeni zilipangiwa kufanyika kwa muda wa wiki moja pekee. Ili kuwezesha wagombea, hasa wa nafasi za uenyekiti wa mitaa na vijiji kufanya kampeni kwa ufanisi, muda wa kampeni usipungue wiki mbili," alisema.

Aliongeza kuwa sheria iweke utaratibu rahisi, wenye ufanisi, uwazi na usawa wa kufanya malalamiko, mapingamizi na rufani kuanzia ngazi ya kata, halmashauri na taifa, ili uchaguzi uwe wa haki.

Vilevile, alisema wanaona kuna haja yawekwe mazingira wezeshi ya watu wenye ulemavu ikiwamo kuwa na karatasi za maandishi ya nukta nundu, na kadri inavyowezekana, mazingira ya vituo vya kuandikishia na kupigia kura yazingatie mahitaji ya watu wenye ulemavu.

"Sheria iweke bayana kipindi maalum cha kuitishwa uchaguzi wa marudio, ili kutibu tatizo la sasa la halmashauri kutoitisha uchaguzi huo kwa kisingizio cha gharama za kuendesha uchaguzi kisijirudie," alisema.

# Mwinyi aahidi kuwapunguzia wananchi hali ngumu ya maisha

**Na Suleiman Rashid Omar,** PEMBA

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imeahidi kukabiliana na hali ya ugumu wa maisha ili kuwapunguzia mzigo wananchi wake.

Makamu Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi, Zanzibar na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, aliyasema hayo Ikulu ya Pagali, Pemba alipozungumza na Wazee wa CCM.

Rais Mwinyi amesema kupanda kwa gharama za maisha kunachangiwa na changamoto nyingi za uchumi duniani, ikiwamo vita, kupanda bei kwa bidhaa za nje na baadhi ya mataifa duniani kuzuia kuuza bidhaa zao kwa mataifa mengine, akitoa mfano nchi ya India iliyozuia kuuza bidhaa zake kwa mataifa mengine duniani.

Alisema, hali hiyo huchangia kuzorotesha uchumi wa mataifa mengi na bei kupanda maradufu.

Aidha, alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itafanya kila linalowezekana kustawisha uchumi na hali za wananchi kwa kuendelea kutekeleza kwa vitendo, Ilani ya Chama cha Mapinduzi na kuimarisha hali ya uchumi kwa wananchi.

Akizungumzia changamoto ya bandari ya mkoani na hali ya kupanda kwa bei za bidhaa nchini, Rais Mwinyi aliwahakikishia wazee na wananchi wa kisiwa cha Pemba kwamba serikali ina nia ya kuleta meli ya moja kwa moja kutoka Bandari ya Mombasa hadi Bandari ya mkoani kwa ajili ya kushusha bidhaa ili kupunguza gharama za maisha na mfumko wa bei za bidhaa hizo.

Pia, Rais Mwinyi aliwaomba wazee kuendelea kuiombea dua nchi ili amani iendelee.

Wazee hao walimpongeza Rais Dk. Mwinyi kwa hatua kubwa ya maendeleo ya nchi ilivyopiga ndani ya muda mfupi.

Aidha, wazee hao walipongeza hatua ya serikali kuendelea kuwalipa pensheni jamii, na kumshukuru, Rais Mwinyi kwa kuwaongezea kima cha pensheni hiyo.

Pia, walimpa pole Rais Mwinyi kwa msiba wa baba yake mzazi uliotokea hivi karibuni.

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA WA KUUZWA KWA MALI ZA KAMPUNI YA UJENZI YA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**

Kampuni ya Ujenzi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yenye namba za usajili Z0000067328 inaendelea na taratibu za kufilisiwa. Hii ni kufuatia azimio la kuifunga Kampuni hiyo kwa hiari lililopitishwa na Bodi ya Wakurugenzi katika kikao kilichofanyika tarehe 21 Juni 2023. Kama sehemu ya mchakato wa kuifunga Kampuni, Wafilisi wa Pamoja walioteuliwa kuongoza mchakato wa kufilisi wanakusudia kuuza mali za Kampuni hiyo kupitia mnada wa hadhara utakaofanyika Jumatano tarehe 3 Aprili 2024 katika eneo la Binguni-Unguja na katika kituo cha Wajasiriamali Kipitacho kilichopo Pemba. Baadhi ya mali zitakazouzwa ni pamoja na;

**Matirio ya ujenzi:** Mchanga, mbao, matofali, mabati, misumari, vifaa vya mabomba, kokoto, vifaa vya umeme, n.k.

**Vifaa vya Ujenzi:** Mashine ya kuchanganya Saruji(Concrete Mixer), Mashine ya kushindilia (Gasoline Tamping Rummer), Mashine ya kushilindilia zege (Concrete Vibrator), Kifaa cha kusambaza umeme Extension Reel (Tronic 220v-240)13A), Kifaa cha kukata chuma (Forged Steel Bar Cutting (model no: 50N/ 28)), Mashine ya kushindilia ardhi (Roller Compactor), Nyundo ya kuvunjia na kutobolea (Breaking Hammer, Hammer Drill and Breaking), Mashine ya kuchomea chuma (Welding Machine), vifaa vya kujilinda (Personal Protective Equipment) n.k.

**Pikipiki:** Aina ya Boxer.

**Kwa maelezo zaidi, tafadhali wasiliana na:**
**Wafilisi wa Pamoja**
**Kampuni ya Ujenzi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar**
**Barua pepe: straton@auditaxinternational.co.tz na khalfai@auditaxinternational.co.tz**
**Simu: +255 719 878 490**

# Mwanasheria LHRC adaiwa anatishiwa usalama

**Na Enock Charles**

KITUO cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), kimedai mwanasheria wake, Joseph Oleshangay, anayeishi jijini Arusha, ametishiwa usalama na watu wanaojitambulisha kuwa wanatoka katika Jeshi la Polisi nchini.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi Mtendaji wa LHRC, Dk. Anna Henga, alisema hali ya mwanasheria huyo imekuwa hatarini kwa muda mrefu tangu 2023 kutokana na watu hao kumfuata mpaka nyumbani kwake kumuulizia bila kutoa sababu zozote.

"Hali ya usalama wa Joseph imekuwa hatarini kwa muda mrefu tangu 2023 na amekuwa anafuatiliwa ikiwamo kupigiwa simu na watu wanaomtafuta. Wengine wakijitambulisha ni Askari wa Jeshi la Polisi," alisema.

Inadaiwa Machi 14 mwaka huu, Joseph alipata taarifa ya kufuatiliwa na watu wanaodaiwa kuwa wanatoka katika vyombo vya dola, hivyo kulazimika kuchukua tahadhari.

"Usiku wa kuamkia Machi 15, watu waliosema bila vitambulisho ni polisi walifika nyumbani kwake na kumkuta mke wake na kumwulizia Joseph bila kutoa sababu za kumtafuta," alisema Henga.

Alisema mbali na watu hao kumkosa Joseph nyumbani kwake, waliweka kambi eneo la nyumbani kwa siku nne bila mafanikio.

Anna alisema matukio yote hayo yamekuwa yakimtia hofu Joseph pamoja na familia yake kwa sababu amekuwa akiwindwa kwa muda mrefu, huku vitisho anavyopewa vikimsababishia kukosa uhuru wa kufanya kazi zake kama mwanasheria na wakili wa masuala ya ardhi.

Dk. Henga alisema baada ya kuona ujumbe mitandaoni kuwa Joseph ni mtu hatari walishangazwa sana japo hawakupuuzia na kwamba wanaendelea kufuatilia na watachukua hatua stahiki pale watakapojiridhisha usalama wake, familia yake, jamii ya wamasai wanaoishi Ngorongoro na wafanyakazi wenzake wa kituo hicho.

"Wakili Joseph Oleshangay ni Mmasai kwa asili, amezaliwa na kukulia katika Kata ya Endulen wilayani Ngorongoro na kituo hicho. Kutokana na taaluma na nafasi yake ya kazi amekuwa akitoa msaada wa kisheria na ushauri kwa jamii yake ya kimasai hasa kwa wale wanaoishi ndani ya Mamalaka ya Ngorongoro (NCAA).

"Tangu mwaka 2022 serikali imekuwa ikiendelea kuwahamisha wananchi kutoka eneo la Ngorongoro na serikali imekuwa ikiliita 'la hiari', Joseph amekuwa akiisaidia jamii yake kuhusu uelewa wa zoezi hilo," alisema.

Alipotafutwa kuhusu madai hayo, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Justine Masejo, alipokea mtu aliyejitambulisha kuwa ni msaidizi wake na kusema bosi wake alikuwa kwenye kikao, hivyo atafutwe baadaye. Hata hivyo, alipotafutwa baadaye, simu iliita bila kupokewa.

# Wawili wafa ajali mabasi kugongana na lori

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MAGARI mawili ya abiria yameteketea kwa moto baada ya kugongana na kusababisha vifo vya watu wawili na kujeruhi watatu.

Ajali hiyo ilitokea jana katika eneo la Mlandizi barabara ya Dar es Salam - Morogoro majira ya saa 10:15 alfajiri.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Pius Lutumo, alisema ajali hiyo imetokea baada ya gari lenye namba za usajili T668 DTF Scania la Kampuni ya Saul likiendeshwa na Idd Aloyce kugonga ubavuni lori la mafuta.

Kamanda Lutumo alisema basi liligonga lori hilo lililokuwa na mafuta ya petroli lenye namba za usajili RAF 672 N na tela RL 2594 aina ya Howo likitokea Dar es Salam likiendeshwa na Mushimana Musiyimana lililokuwa limesimama kupisha gari lililokuwa linakuja mbele yake.

Basi la Saul ambalo liliongozana na basi lingine aina ya Golden Deer la Kampuni ya New Force lenye namba za usajili T 175 DZU likiendeshwa na Burton Jacob (33) nalo liligonga kwa nyuma basi la Saul na kusababisha vifo vya watu wawili na majeruhi watatu.

Lutumo alisema waliofariki dunia katika ajali hiyo ni Salim Days (50) mkazi wa Mbozi, Farida Idrisa (26) mkazi wa Tabata jijini Dar es Salam na Kyambile Godfrey mkazi wa Uyole mkoani Mbeya.

Alisema baada ya ajali hiyo, Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji wakiwa katika harakati za kuwatoa marehemu waliokuwa wamenasa, ghafla moto uliwaka kutokana na petroli iliyokuwa inatoka kwe tangi la mafuta.

Hata hivyo, alisema moto huo ulidhibitiwa na kuwatoa marehemu waliokuwa wameteketea kwa moto na moto ulilipuka tena toka chumba cha tangi na kusababisha majeraha kwa askari wawili wa zimamoto.

Aliwataja askari hao kuwa ni Koplo Hamis Kungwi na Koplo Elias Bwire ambao walipelekwa kupatiwa matibabu katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Tawi la Mloganzila.

Kamanda Lutumo alisema chanzo cha ajali hiyo ni uzembe wa madereva wawili kushindwa kuchukua tahadhari kwa kuyapita magari mengine pia kushindwa kutunza umbali kati ya gari moja na lingine yakiwa yanafuatana.

Alisema uchunguzi wa awali umebaini chanzo cha moto ni hitilafu ya injini katika basi la Saul lililokuwa limekita chini baada ya kugonga gari lingine na kulipua petroli wakati wa uokoaji.

## TAARIFA KWA UMMA

airtel money

### Wadhamini Waliosajiliwa wa Airtel Money Trust Fund

Imetolewa kwa mujibu wa kanuni ya 33(b) ya Kanuni za Fedha za Kielektroni , 2015

**A** TAARIFA YA USIMAMIZI WA FEDHA HADI DISEMBA 31, 2023

| | 2023 TZS' 000 | 2022 TZS' 000 |
|---|---|---|
| **Mali** | 355,758,422 | 272,891,833 |
| Salio lililopo katika mfuko wa Airtel Money | 355,758,422 | 272,891,833 |
| **Jumla ya thamani ya Mali** | | |
| **Uwiano na utoshelevu wa mtaji na dhima Mtaji** | | |
| Hazina iliyokusanywa | - | - |
| **Jumla ya Mtaji** | - | - |
| **Mgawanyiko wa mali** | | |
| Amana za wateja | 326,905,591 | 263,885,241 |
| Dhima ya mawakala, wafanyabiashara na wateja | 7,890,730 | 7,037,666 |
| Dhima nyingine | 962,101 | 1,968,926 |
| Jumla ya dhima | 335,758,422 | 272,891,833 |
| Jumla ya mtaji na dhima | 335,758,422 | 272,891,833 |

**B** TAARIFA YA MAPATO

Airtel Money Trust Fund, ni taasisi ya wadhamini ambapo uendeshaji wake unasimamiwa na Kampuni ya Airtel Money Tanzania Ltd, hivyo AM Trust Fund haina mapato.

**C** TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA MWAKA ULIOISHIA TAREHE 31 DISEMBA 2023

| | 2023 TZS' 000 | 2022 TZS' 000 |
|---|---|---|
| **Mtiririko wa Fedha kutokana na shughuli za uendeshaji kabla ya mabadiliko ya mtaji wa uendeshaji** | - | - |
| Faida kabla ya kodi | - | - |
| **Kuongezeka (Kupungua) kwa Amana za wateja** | 63,020,351 | 49,875,887 |
| Kuongezeka (Kupungua) kwa Dhima yamawakala, wafanyabiashara na wateja | 853,064 | (251,091) |
| Ongezeko la dhima nyingine | (1,006,826) | 880,616 |
| **Mtiririko wa fedha halisi unaotokana na (hutumika katika) shughuli za uendeshaji** | 62,866,589 | 50,505,412 |
| Ongezeko la jumla / (punguzo) kwa usawa uliofanyika chini ya Airtel money Trust | 62,866,589 | 50,505,412 |
| Salio la Airtel Money Trust mwanzoni mwa mwaka | 272,891,833 | 222,386,421 |
| Salio la Airtel Money Trust mwishoni mwa mwaka | 335,758,422 | 272,891,833 |

**D** TAARIFA YA MABADILIKO KWA MWAKA ULIOISHIA DISEMBA 31, 2023

| | Mtaji wa hisa TZS' 000 | Akiba ya mtaji TZS' 000 | Jumla TZS' 000 |
|---|---|---|---|
| Mpaka kipindi cha Januari 1, 2023 | - | - | - |
| Jumla ya hasara mpaka Tarehe 31, 2023 | - | - | - |
| **Tarehe 31, Disemba 2023** | - | - | - |
| Mpaka kipindi cha 1 Januari 2022 | - | - | - |
| Jumla ya hasara kwa kipindi cha mpaka Januari 1 2022 Tarehe 31 Disemba 2022 | - | - | - |
| **At 31 December 2022** | - | - | - |

**E** MAELEZO YA MWAKA ULIOISHIA DISEMBA 31, DISEMBA 2023

Katika utayarishaji wa taarifa za fedha, sera thabiti ya uhasibu imetumika kama ilivyotumika kwenye taarifa ya Fedha iliyokaguliwa ya mwaka uliopita. (Kama kulikuwa na mabadiliko katika mwaka huu, mabadiliko yameelezewa kama ilivyo kwenye IAS 8).

| Jina & Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| Andrew Rugamba **Mkurugenzi** | | 31/01/2024 |
| Rajesh Chawla **Mkuu wa kitengo cha Fedha** | | 31/01/2024 |
| Glory Minja **Mkuu wa kitengo cha Ukaguzi wa Ndani** | | 31/01/2024 |

Sisi wakurugenzi tuliotia saini hapo, tunathibitisha uwakilishi wa kiuaminifu kwa waliotajwa hapo juu. Tunakubali kuwa taarifa hizi zimethibitishwa na sisi kwa imani na ujuzi thabiti, zimetayarishwa kulingana na Sheria ya kimataifa ya masuala ya fedha inayohitajika kutumika kama sheria ya mfumo wa malipo,2015 na imewasilisha maoni ya kweli na ya haki.

| Jina & Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| Judge Joseph Sinde Warioba **Mdhamini** | | 31/01/2024 |
| Dr. Evelyn Mweta Richard **Mdhamini** | | 31/01/2024 |

Download on the App Store | ANDROID APP ON Google play

Vigezo na Masharti kuzingatiwa

HARAKA.SALAMA.BILA MIPAKA.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Usafiri treni ya umeme utumike kuleta mageuzi sekta ya uchukuzi

**SEKTA** ya usafirishaji ni muhimu katika kukuza uchumi na vilevile mageuzi ya maendeleo nchini.

Usafiri unapokuwa wa uhakika na kuaminika huvutia pia wafanyabiashara wa mataifa mengine kuutumia.

Usafiri wa treni ya kisasa inayotumia umeme, unatarajiwa kuleta mageuzi makubwa nchini utakapoanza rasmi kutumika.

Jambo la kwanza utaokoa muda mwingi kwa wasafiri kukaa barabarani kufika wanakokwenda na vilevile utaokoa uharibifu wa miundombinu ya barabara pale malori yanapobeba mizigo mizito.

Hivi karibuni Kamati ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC) imeeleza kuridhishwa na majaribio yanayoendelea ya treni ya umeme katika reli ya Standard Gauge kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Augustine Vuma, amesema kamati hiyo pia imejiridhisha kuwa thamani ya fedha zilizotumika katika mradi huo zimetumika sawa na hatua za ununuzi zilifuatwa.

Hata hivyo, ombi la Kamati hiyo ni kuutaka uongozi wa TRC kulinda mradi huo ili kuhakikisha unakuwa endelevu, pia kamati hiyo imetaka mkandarasi kukamilisha mradi kwa wakati kulingana na makubaliano ya kimkataba.

Mradi huo kwa mujibu wa Mwenyekiti wa Kamati hiyo, umetoa ajira za moja kwa moja 30,000 na ajira 150,000 zisizo za moja kwa moja hadi sasa na kwamba jamii ina jukumu kubwa la kuhakikisha miundombinu yote inalindwa.

Mwenyekiti amekumbusha jambo la msingi la jamii kulinda miundombinu ya mradi huo ili uweze kudumu kwa muda mrefu na kuleta faida nchini.

Kwa watu ambao wameshasafiri katika nchi zingine duniani zinazotumia usafiri huo, watakubaliana na mwenyekiti kuhusu jamii kulinda miundombinu hiyo.

Uharibifu mara kwa mara hufanywa na jamii kwa kutokuwa na uzalendo au kuhujumu miundombinu kwa makusudi.

Hili linaonekana hata kwenye barabara za kisasa zilizojengwa nchini kwa uharibifu unaofanyika kung'olewa kwa kingo za madaraja na alama za barabarani kwa lengo la kuchukua vyuma na kwenda kuviuza kama vyuma chakavu.

Miradi kama hii inalindwa kuanzia njia zinazotumika mpaka vyombo vinavyobeba abiria. Kwa mfano kwenye baadhi ya nchi ambazo zinatumia usafiri wa treni kama wa umma, kuna masharti yanayokataza abiria kula au kunywa aina yoyote ya kinywaji anapokuwa ndani ya usafiri huo.

Abiria yeyote atakayekwenda kinyume na onyo hilo anatozwa faini kubwa na sheria inatekelezwa.

Msafiri yeyote awe mwenyeji au mgeni ni lazima anapoingia kwenye usafiri huo asome masharti kuepuka kupigwa faini.

Hatua hiyo imesaidia watu kufuata sheria na vilevile kuwa wasimamizi wa wengine wanaojisahau.

Hapa nchini pia hilo linawezekana kama kutakuwa na ufuatiliaji na utekelezaji ili kulinda miradi hiyo mizuri itakayosaidia nchi kuongeza mapato.

Mwenyekiti wa Bodi ya TRC, Ally Karavina, amehakikisha kuwa majaribio yanayoendelea yamezingatia taratibu zote za uhandisi.

Habari njema ni kuwa shughuli hizo zinaanza mwishoni mwa Julai mwaka huu.

Mkurugenzi Mkuu wa TRC, Masanja Kadogosa amewahakikishia wananchi kutangaza gharama za nauli kama ilivyoelekezwa na serikali.

Majaribio kutoka Morogoro hadi Dodoma yataanza wakati wowote mwezi ujao na wahandisi walikuwa wakikamilisha baadhi ya mitambo ili kuruhusu treni hiyo kupita.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Safi sana PASADA, hizo nyendo zenu zimewaokoa wenzetu wengi

Na Halfani Chusi

**SHIRIKA** lililo Chini ya Jimbo Kuu Katoliki la Dar es Salaam (PASADA), Linalojihusisha na utoaji wa huduma kwa watu wanaoishi na Virusi vya Ukimwi, kuanzia Aprili. mwaka jana hadi Desemba, lilibua wagonjwa wa kifua kikuu 919 na kuwapatia matibabu bure katika mikoa ya Pwani na Dar es Salaam.

Shirika hilo liliibiua wagonjwa kupitia utambuzi na uchunguzi uliofanywa kupitia mradi wa wake uitwao 'Stop TB Partnership.'

Mwishoni mwa wiki iliyopita mkoani Dar es Salaam na Meneja Mradi wa TB Pasada, Jacquline Mwaipaja, anasema katika idadi hiyo kati yao 111 walikuwa watoto wenye umri chini ya miaka 15, pia kuna wengine 256 waliogundulika na maambukizi ya Virusi vya Ukimwi na Kifua Kikuu.

Pia, akasema kwa mwaka uliopo, walifanikiwa kuwafikia wagonjwa wengine 622, hata wakawapatia huduma za kiugunduzi na matibabu ya kifua kikuu, akiwa na msisitizo alipata changamoto wagonjwa wengi walikuwa hawana gharama ya kulipia kipimo cha mionzi (X - Ray).

Ni jambo linaloungwa mkono na Mkurugenzi wake Mtendaji, Cayus Mrina, anayetamba kwamba kufanikiwa katika mradi huo, ni matokeo ya serikali ya sasa, kuweka mazingira wezeshi kati ya serikali na mashirika binafsi.

"Amejitahidi kuhakikisha huduma za afya zinafika mahali kote, kila mahali kuna vifaa na huduma za afya, tunatoa huduma za kimwili na kiroho ndio maana kauli mbiu yetu inasema 'roho yenye afya na mwili wenye afya' kwa hiyo watu wanapata huduma zote," anafafanua.

Anarejea historia, shirika hilo lilianzishwa mwaka 1992 kwa lengo la kutoa huduma kwa watu wanaoishi na Virusi vya Ukimwi, akikumbushia kipindi hicho kulikuwapo wagonjwa wengi, ndipo jitihada za mapadri zikazaa kuwapo PASADA.

"Mapadri Wamisionari waliokuwa wanafanya kazi ya kuhudumia wagonjwa kiroho, wakaona kuna haja ya kuungana pamoja kupata sehemu ya kituo cha kuhudumia wagonjwa," anasema

Anasema mpaka sasa kuna vituo 25 katika mkoa wa Pwani na Dar es Salaam, ambavyo vinatoa huduma hizo, akisistiza kwa sasa wanafanya kazi hizo kwa kasi kubwa ili kuchangizа malengo ya serikali.

Ni jambo linaloungwa mkono pia na mganga mkuu wa halmashauri ya Temeke aliyekuwa mgeni rasmi kwa niaba ya serikali Jonasi Lulandala, anayeahidi kuyafanyia kazi maombi yao ya kushusha gharama katika kipimo cha mionzi.

"Nitalifikisha kwa Mganga Mkuu wa Mkoa nione namna gani tutalifanyia kazi, ninawapongeza PASADA, kwa kazi mnazozifanya katika jamii, kwa kutibu wagonjwa na kuzuia maambukizi mapya, kwa hiyo kuna kazi kubwa ya kufanya kaungalia kwa nini wagonjwa wanaongezeka," anasema

Pia, walikuwapo wanufaika wa mradi huo waliotibiwa bure na kupona kabisa. Shabani Salumu, ni miongoni mwao akisema alikuwa mwathirika wa kifua kikuu alifikiwa na PASADA na kupatiwa matibabu na sasa amepona kabisa.

"Mara ya kwanza walinikuta kijiweni mimi ni mwathirika wa dawa za kulevya, wakanihoji wakachukua makohozi yangu, wakaenda kuyapima.

"Siku mbili baadaye wakanifuata, wakasema makohozi hayajaonyesha kama unakifua kikuu, wakaniambia inabidi tukupime kwa mionzi nikawaambia gharama hizo mimi sina wakasema tutakusaidia.

"Baada ya hapo wakanifanyia hicho kipimo, nikagundulika nina tatizo la kifua kikuu na sasa ninatumia dawa naendelea vizuri ninawashukuru sana," akatamka.

Mnufaika mwingine, Hemedi Jumanne anasema amesumbuliwa sana na kifua kikuu kwa zaidi ya miezi miwili, alipopima makohozi katika hospitali mbalimbali, hayakuonyesha ugonjwa.

"Katika matembezi yangu nikakutana na PASADA, nikawasimulia wakaniambia inabidi nipime kipimo cha mionzi nikawaambia sina hela wakaniambia tutakupa msaada.

"Waliponipima nikakutwa nina kifua kikuu ninawashukuru sana waendelee na huduma hii kwa sababu huko mtaani wapo wengi wanaoumwa, lakini hawana uwezo wa kifedha" anashauri

Ni jambo linalopaswa kuungwa mkono kusaidia wenye uhitaji katika jamii kwenye nyanja mbalimbali sio afya pekee wapo wanaohitaji mitaji kukuza biashara, wajane, yatima na wenye ulemavu.




Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usafiri wa Anga nchini (TCAA), Hamza Johari (katikati), akiongoza menejimenti ya Mamlaka hiyo, kukabidhi zawadi za maandalizi ya Sikukuu ya Eid kwa watoto wanaolelewa katika kituo cha Busara cha Ukonga Banana, baada ya kuwafuturisha, jijini Dar es Salaam, juzi. **PICHA: DICKSON MULASHANI**

# ATCL yaanza kukabiliana na hewa ya kaboni

**Na Vitus Audax,** MWANZA

KUTOKANA na safari za anga kuwa sehemu ya uzalishaji wa hewa ya kaboni kwa asilimia 2.4 hadi 2.5 nchini, kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) imefadhili mradi wa utunzaji mazingira wa Twiga wa Kijani kwa zaidi ya Sh. milioni 124.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa kampeni hiyo jana inayosimamiwa na shirika lisilokuwa la kiserikali la Wezesha Binti na Mama Mjasiriamali (WBM), Mkurugenzi Mtendaji wa ATCL, Ladislaus Matindi, alisema hatua ni juhudi za kampuni hiyo kupunguza ongezeko la joto na hewa ya kaboni nchini.

"Uchangiaji wa kaboni unaosababishwa na usafiri huu, unatarajiwa kuongezeka zaidi ifikapo 2030 hadi kufikia asilimia tano huku ukichangia pia ongezeko la joto duniani (global warming)' kwa asilimia tano," alisema.

Matindi alisema kampuni inaendelea na mapambano dhidi ya mabadiliko ya tabianchi kwa kujikita zaidi katika matumizi ya mifumo rafiki ya injini pamoja na kufadhili miradi ya utunzaji wa mazingira kwa fungu la zaidi ya Sh. milioni 124 kwa mwaka mmoja.

Akizindua kampeni hiyo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Selemani Jafo, alisema kampeni hiyo itakuwa sehemu ya utekelezaji wa kampeini ya iliyoanzishwa mwaka 2022 ya Soma na Mti.

Jafo alisema katika hatua hiyo ya kupandikiza elimu ya upandaji miti kwa wanafunzi ikiambatana na shughuli za upandaji miti inatakiwa kuwa ili kupunguza uchafuzi utokanao na hewa ya kaboni pamoja na mabadiliko ya tabianchi.

Aliziagiza halmashauri kutekeleza lengo la upandaji miti milioni 1.5 kama yalivyo maelekezo ya serikali kwa kushirikiana na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS).

Pia alizitaka halmashauri zote 184 kutenga bajeti kwa ajili ya kuwawezesha kinamama na vikundi mbalimbali vya uzalishaji miti ili kuongeza idadi ya miti nchini na kukabiliana na ongezeko la joto duniani.

Mkurugenzi Mtendaji wa WBM, Ratifa Mohamed, alisema kampeni hiyo inalenga kutoa elimu ya utunzaji wa mazingira kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari 60 pamoja na kupanda miti 6,000 katika mikoa sita.

Alitaja mikoa hiyo kuwa ni Mwanza, Kagera, Kilimanjaro, Mbeya, Arusha na Mtwara na kwamba kila mkoa utapanda miti 1,000 kwa shule 30 za msingi na 30 za sekondari.

# Adaiwa kujiua kwa sumu kituo cha polisi

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MCHIMBAJI Madini, Gamalieli Munisi 'Chinga' (48), mkazi wa Muriet, mkoani hapa, anadaiwa kujiua kwa kunywa sumu akiwa viunga vya Kituo cha Polisi Murieti, alikoitwa kwenye dawati la jinsia.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP), Justine Masejo, alithibitisha tukio hilo na kusema Munisi anadaiwa kunywa sumu Machi 20, mwaka huu na kuanguka katika viwanja vya polisi.

Alisema baada ya kufanya hivyo, juhudi zilifanyika kumwahisha Hospitali ya Murieti ili kuokoa maisha yake, lakini alifariki dunia siku iliyofuata.

Kamanda Masejo alidai Munisi alikuwa na mgogoro wa muda mrefu na mkewe, lakini siku hiyo aliitwa polisi kwa ajili ya usuluhishi na alipofika katika viunga vya kituo cha polisi, alianguka chini.

Mmoja wa mashuhuda eneo la polisi, Anneth Asenga, alidai kuwa Munisi baada ya kufika kituo cha polisi, walianza mahojiano kwenye dawati la jinsia, lakini hakuridhika na namna alivyokuwa akihojiwa na askari hao, akatishia kunywa sumu.

"Akiwa katika mahojiano, alikerwa na hatua ya askari waliokuwa kwenye dawati na kutishia kunywa sumu ndipo mmoja ya askari hao alimwambia kuwa 'usitutishe na kama unataka kunywa sumu, nenda kanywe'.

"Baada ya kuelezwa hivyo, jamaa alitoka kwa hasira na kutoa kitu mfukoni na kubugia mdomoni kisha baadaye alianguka," alidai.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Field Force, Veronica Guta, alipoulizwa kuhusu tukio hilo, alisema hakuwahi kushuhudia mgogoro kati ya Munisi na mkewe, lakini amekuwa anasikia wana mgogoro.

Alisema siku ya tukio, wawili hao waliitwa Kituo cha Polisi Murieti, dawati la kijinsia, kwa ajili ya usuluhishi lakini hakuna aliyejua kuwa Munisi alikuwa na sumu mfukoni.

Mwili wa Munisi tayari umezikwa nyumbani kwao, Hai mkoani Kilimanjaro.

## KABWELA

Na Fadhili Mohammed



# Wataka udhibiti rushwa, ufisadi bajeti mpya

**Na Zanura Mollel**

BAADHI ya wakazi wa Dar es Salaam wameshauri serikali kuweka mpango mkakati wa kudhibiti rushwa na ufisadi kwenye bajeti ya mwaka 2024/25 itakayoanza kutekelezwa Julai Mosi, mwaka huu.

Vivian Robert, mkazi wa Mabibo na Makamu wa Rais Serikali ya Wanafunzi ya Chuo Kikuu Mzumbe, alisema kumekuwa na tabia ya baadhi ya watu wenye nguvu ya kifedha na madaraka kuhodhi fedha za miradi kwa manufaa yao na kusahau lengo la fedha hizo. Alisema rushwa imechangia baadhi ya fedha za miradi kutowafikia wananchi kama ilivyotengwa. Pia alisema kumekuwapo matumizi yasiyo na tija kwa fedha za serikali kutoka kwa baadhi ya viongozi katika ngazi za wizara na serikali za mitaa.

Kuhusu matarajio yao katika bajeti hiyo, Venance Peter, mkazi wa Mabibo, alisema huduma kwa wanawake wajawazito na watoto iwekwe wazi kama ni bure au ya malipo lakini akasema matamanio yake iwe bure.

Alisema Katika upande wa miundombinu ya barabara kumekuwepo na changamoto ya muda mrefu kwa ubovu wa barabara hususani vijijini na mijini hali hiyo inakwamisha shughuli za kiuchumi kwa wananchi.

"Wakati mwingine wajawazito wanashindwa kufika katika vituo vya kutolea huduma ya uzazi kutokana na miundombinu kutokuwa rafiki na kusababaisha magari kutopitika," alisema Peter.

Alisema maendeleo ya taifa ni pamoja na uhakika wa upatikanaji wa umeme, hivyo bajeti hiyo ingeangazia zaidi suala hilo kutokana na wafanyabiashara wengi hivi karibuni kulalamika kuhusu changamoto ya huduma hiyo na kusababisha kuzorota kwa shughuli za uzalishaji mali.

"Wafanyabiashara wanalalamika biashara zao kusimama hata kwa zaidi ya wiki moja kutokana na mgawo wa umeme. Tunatambua kuwa wengi wao hutegemea nishati hiyo hususani maeneo ya viwandani yanayofanya uzalishaji zaidi," alisema Peter.


Pia alisema sekta ya kilimo inapaswa kuangaliwa kwa mapana kwa kuhakikisha wakulima wadogo ambao asilimia kubwa ni wanawake, wanapatiwa pembejeo za kilimo mapema ili kwenda sawa na misimu ya kilimo.

Alisema upatikanaji wa masoko ya uhakika kwa wakulima ndani na nje ya nchi utasaidia kuwainua kiuchumi katika bajeti ya ngazi za familia na kupunguza umaskini wa mtu mmoja mmoja na makundi kwa ujumla.

Mwanafunzi wa Chuo cha Mipango Dodoma, Swaumu Maftah, alisema mikopo ya asilimia 10 kutoka katika makusanyo ya ndani ya halmashauri inapaswa kufanyiwa maboresho ili kuondoa ukakasi kwa wanufaika.

"Mikopo hii natarajia bajeti itaangazia kwa mapana na kuhakikisha inawafikia walengwa,tumeona vijana walionufaika na fedha hizi,kinachoitajika ni uwazi na haki katika utoaji." alisema Maftah.

Ofisa Progamu Mwandamizi wa Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), Zainab Mmary, alisema wananchi wanapaswa kushiriki katika mchakato wa mapendekezo ya bajeti kuanzia ngazi ya vijiji ili kutambua na kuibua miradi mbalimbali wanayohitaji katika maeneo yao.



Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Serikali (PAC), Japhet Hasunga (katikati), akizungumza na Katibu Mkuu wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mhandisi Anthony Sanga (kulia) na Naibu Waziri wa wizara hiyo, Geophrey Pinda wakati wa ziara ya kamati hiyo ya kukagua hatua iliyofikiwa katika Utekelezaji wa Mradi wa Uboreshaji Usalama wa Milki za Ardhi katika Mji wa Nzega, mkoa wa Tabora juzi. **PICHA: WANMM**

# Wizara yapongezwa miradi uboreshaji ardhi

**Na Munir Shemweta,** NZEGA

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) imeipongeza Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa utekelezaji wa Mradi wa Uboreshaji Usalama wa Milki za Ardhi (LTIP) katika Halmashauri ya Mji wa Nzega mkoani Tabora.

Pongezi hizo zilitolewa juzi wilayani hapa na Makamu Mwenyekiti wa PAC, Japhet Hasunga, wakati wa ziara ya kamati kukagua hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa LTIP kwenye halmashauri hiyo.

Mradi wa LTIP katika Halmashauri ya Mji wa Nzega umepewa lengo la kurasimisha vipande vya ardhi 20,000 na kuongeza alama za msingi za upimaji 14.

"Niwapongeze kwa kazi hii mliyoamua kuifanya. Tangu tupate uhuru tumekuwa na changamoto za ardhi kuanzia kutambua, kupima, kurasimisha nakadhalika na kumekuwa na shida" alisema.

Hasunga alisema Rais Samia Suluhu Hassan ameamua kutoa fedha nyingi za mradi wa LTIP na Bunge kuidhinisha na kwa Halmashauri ya Mji wa Nzega, Sh. bilioni 1.4 zimeidhinishwa kwa ajili ya kata tano, hivyo wananchi watumie fursa ya kutambuliwa maeneo yao na hatimaye kupatiwa hati kupitia mradi huo.

Alisema PAC itakwenda kupima thamani ya fedha zilizopitishwa na bunge pale tu wananchi watakapokuwa na hati.

"Msipopata hati, hii mingine yote ni michakato. Sisi hatuhitaji michakato tunataka kuona watu wangapi wana hati," alisisitiza Hasunga.

Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Geophrey Pinda, amesema wizara ina uhakika michakato yote itakapokamilika katika mji wa Nzega, hatimilki za ardhi zitatolewa kwa wananchi.

Kwa mujibu wa Pinda, utekelezaji wa LTIP utatoa hatimilki 1,500,000 za ardhi kwa maeneo yote yanayopotiwa na mradi.Katibu Mkuu wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mhandisi Anthony Sanga, alisema kazi iliyofanyika kwa Halmashauri ya Mji wa Nzega mpaka sasa imefikia asilimia 55 na fedha zilizotolewa ni asilimia 39.

Mradi wa Uboreshaji Usalama wa Milki za Ardhi (LTIP) unatekelezwa kwa mkopo wenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 50 kutoka Benki ya Dunia kwa kupindi cha miaka mitano katika halmashauri 58 nchini.

Mradi huo unalenga kuboresha utawala na usimamizi wa ardhi nchini pamoja na kuongeza usalama wa milki za ardhi kwa wananchi.

# Wabunge wakunwa na majaribio SGR

**Na Frank Monyo**

KAMATI ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC) imeeleza kuridhishwa na majaribio yanayoendelea ya treni ya umeme katika reli ya kisasa (SGR) kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro.

Akizungumza jana baada ya majaribio hayo, Makamu Mwenyekiti wa PIC, Augustine Vuma, alisema kamati hiyo pia imejiridhisha kuwa thamani ya fedha zilizotumika katika mradi huo zimetumika sawa na hatua za manunuzi zilifuatwa.

"Napenda kuipongeza serikali kwa kutoa fedha kwa wakati ili kuhakikisha mradi unakamilika. Shughuli zitakapoanza, mradi huu utapunguza gharama za usafirishaji wa mizigo kwa asilimia 40.

"Natoa wito kwa uongozi wa TRC kuulinda mradi huu na kuhakikisha unakuwa endelevu. Pia tunautaka uongozi wa TRC kuhakikisha mkandarasi anakamilisha mradi kwa wakati kulingana na makubaliano ya kimkataba," alisema.

Vuma aliongeza kuwa mradi huo umetoa ajira za moja kwa moja 30,000 na ajira 150,000 zisizo za moja kwa moja hadi sasa hivyo jamii ina jukumu kubwa la kuhakikisha miundombinu yote inalindwa.

Mwenyekiti wa Bodi ya TRC, Ally Karavina, alisema majaribio yanayoendelea yamezingatia taratibu zote za uhandisi.

"Tutatekeleza maagizo ya serikali ya kuhakikisha shughuli hizo zinaanza mwishoni mwa Julai mwaka huu," alisema.

Mkurugenzi Mkuu wa TRC, Masanja Kadogosa, aliwahakikishia wananchi kuwa shughuli hizo zitaanza mwishoni mwa Julai, mwaka huu, ikiwa ni pamoja na kutangaza gharama za nauli kama ilivyoelekezwa na serikali.

Alisema majaribio kutoka Morogoro hadi Dodoma yataanza wakati wowote mwezi ujao na kuongeza kuwa wahandisi walikuwa wakikamilisha baadhi ya mitambo ili kuruhusu treni hiyo kupita.



# CHADEMA yatangaza maandamano mengine ya mikoa

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), kimetangaza kuanza tena maandamano ya amani ngazi ya mikoa, safari hii ikianza na Moshi Mjini mwishoni mwa Aprili mwaka huu.

Maandamano hayo yanalenga kuendelea kuishinikiza serikali kuja na mpango wa dharura wa kukwamua makali ya maisha wanayopitia Watanzania kwa sasa.

Jana, Mwenyekiti wa CHADEMA, Kanda ya Kaskazini, Godbless Lema, alisema maandamano hayo yatawahusisha viongozi wa kitaifa, akiwamo Mwenyekiti wa chama hicho Taifa, Freeman Mbowe.

"Moshi tunakuja kwenye maandamano mwisho wa mwezi wa nne, mimi nitakuja kwenye maandamano hayo. Mwenyekiti Mbowe na yeye atakuja kuandamana Moshi.

"Tutakapotangaza tunaomba njooni barabarani.

Huu ni mji unaowakilishwa na wajanja, hatuwezi kuwa na wajanja halafu hatuwezi kuja kwenye maandamano." Alisema Lema.

Katika mkutano huo, pamoja na mambo mengine Lema alisema mabadiliko ya tabianchi yanayoitikisa dunia kwa sasa yanakwenda kusababisha nchi nyingi za Afrika kuwa na njaa.

"Hali inaenda kuwa mbaya sana kwa sababu ya namna tunavyojipanga kuhimili mabadiliko hayo. Tunahitaji viongozi ambao wana maono ya kuacha kusubiri kesho na kuyamaliza leo," alisisitiza.

Katika mkutano wa kuhitimisha ngwe ya pili ya maandamano ya majiji uliofanyika Februari 26 mwaka huu, Mbowe alisema katika majiji yote waliyofanya maandamano walitembea kilomita 166.

Mbowe aliyataja majiji hayo kuwa ni Mbeya, Mwanza, Dar es Salaam na Arusha.



Meneja wa Mamlaka ya maji na usafi wa mazingira vijijini (RUWASA), wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara, Mhandisi Joanes Martin akielezea faida za mradi wa kuboresha huduma ya maji na usafi wa mazingira vijijini kwa ubia na sekta binafsi, wakati wa mkutano wa wadau wa maji, wilayani humo juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Jeshi la Polisi lakaa mguu sawa kuelekea Sikukuu ya Pasaka

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

JESHI la Polisi limeonya wananchi kujiepusha na vitendo vyovyote vitakavyoathiri imani iliyopo, wakati dunia ikielekea katika sherehe ya Sikukuu ya Pasaka, ambayo itatanguliwa na ibada ya Ijumaa Kuu.

Kwa mujibu wa Msemaji wa Jeshi la Polisi nchini, Naibu Kamishna, David Misime, viongozi wote wa dini watakaoendesha ibada ya usiku katika makanisa yao, wanapaswa kutoa taarifa kwa jeshi hilo katika maneo yao, ili kuimarisha ulinzi na usalama.

"Jeshi la Polisi tumejipanga kikamilifu kuhakikisha sherehe za Sikukuu ya Pasaka zinafanyika katika hali ya amani, utulivu na usalama wa kutosha. Tumejipanga kufanya doria katika mitaa na barabara zote kuu ili kuzuia uhalifu au uvunjifu wowote ule wa amani.

"Kwa viongozi wa madhehebu ya dini za kikristo, ambao watakuwa na ibada ya Ijumaa Kuu, zikiwemo za usiku katika kipindi hiki wasisite kutoa taarifa kwa Jeshi la Polisi ili kuimarisha ulinzi na usalama katika kipindi chote." alisema Kamanda Misime.

Kamanda Misime alisema jeshi hilo litaimarisha ulinzi mkali kwa kufanya doria katika nyumba zote za ibada nchini, wakati wa ibada ya Ijumaa Kuu na Mkesha wa Pasaka, ambayo hukusanya watu wengi mchana na usiku.

Alisema doria hizo zitafanyika kwa siku nne mfululizo usiku na mchana, kuanzia Machi 28 hadi Jumatatu ya Pasaka ya Machi 31. "Niwatake madereva wa vyombo vya moto kuepuka kuendesha vyombo hivyo, wakiwa wamelewa ama kujaza abiria kupita kiasi, alisema.

Pia, aliwataka wananchi kuchukua tahadhari na kujiepusha na tabia ya kuwa na marafiki wa mitandaoni na matapeli wanaojitangaza kuwa wanatoa mikopo kupitia mitandao.

"Niwaombe wananchi kujiepusha na tabia ya kuwa na marafiki kwenye mitandao ya kijamii, ili kuepuka matapeli wanaojitangaza kuwa wanatoa mikopo, kwa njia ya mtandao na kuwatapeli wananchi," alisema. Aidha, alitoa wito kwa wananchi nchini kuendelea kuzingatia kanuni ya kiusalama inayosema 'Usalama unaanza na mimi mwenyewe'.

# KKKT yatamani kuwapo kifurushi bima ya afya wenye ulemavu

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

MKUU wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Askofu Alex Malasusa, amesema kanisa hilo litapaza sauti kuisukuma serikali kuja na kifurushi maalum kwenye Mfuko wa Bima ya Afya ya Taifa (NHIF), kwa ajili ya jamii ya watu wenye ulemavu wa viungo.

Aidha, amesema kifurushi hicho maalum kitawasaidia wenye ulemavu wa viungo, kumudu gharama za uchunguzi, matibabu na ununuzi wa vifaa vya kuwasaidia kujongea.

Askofu Malasusa aliyasema hayo mkoani hapa alipozitembelea na kujionea utendaji wa Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Kaskazini ya KCMC, Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa na Taaluma (Kilimanjaro Clinical Research Institute-KCRI na Shirika la Msamaria Mwema (GSF) zinazomilikiwa na KKKT.

Katika hatua nyingine, alisema anakusudia kuja na mpango maalum wa ziara ya mafunzo ya maaskofu wa dayosisi zote za kanisa hilo nchini, kwenda kujifunza na kupata taarifa za utafiti mbalimbali za magonjwa zinazofanywa na KCRI.

"Ninataka kuongeza uzito kwa KCRI ambacho kiko chini ya KCMC. Nakuja na mpango wa maaskofu wa KKKT, kutembelea taasisi hii na kuona utafiti zinazofanyika.

"KCRI inahitajika kufahamika na wanakanisa, kwa sababu ndiyo taasisi ambayo inategemewa sehemu mbalimbali nchini, kwa kutoa watafiti waliobobea katika kufanya utafiti mbalimbali.

Chuo kinazungumziwa sana, lakini kanisa na wanakanisa wapate kujua kwamba tunafanya utafiti mkubwa sana. Nilikuwa naongea na kijana wangu mmoja kutoka NIMR (Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu), akaniambia miongoni mwa taasisi za utafiti tunazozitegemea ni KCRI. Sasa mara nyingi mnaweza mkawa na kitu, lakini msijivunie." alisema.

Kutokana na umuhimu huo wa KCRI, Askofu Malasusa, alisema kwa mwaka huu atahakikisha maaskofu wote wanafika katika taasisi hiyo na Shirika la Msamaria Mwema kujifunza mambo mbalimbali.

Mkurugenzi wa Hospitali ya KCMC, Prof. Gileard Massenga, aliishukuru serikali kuwapa Sh. bilioni tatu za umaliziaji wa jengo la kutoa huduma za mionzi kwa wagonjwa wa saratani.

Vilevile, Prof. Massenga, alisema kupitia wadau wengine ambao wapo nchini Marekani, pamoja na Shirika la Msamaria Mwema, waliandika andiko lililofanikisha kupata zaidi ya Sh. bilioni 1.5.





# Mbarawa: Mv Mwanza kuanza kazi Juni

**Na Vitus Audax,** MWANZA

WAZIRI wa Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa amehitimisha hatua ya mwisho ya majaribio ya safari ya meli ya Mv.Mwanza 'Hapa kazi tu' na kujiridhisha kuwa ifikapo Juni mwaka huu itaanza kazi rasmi.

Aliyasema hayo jana wakati wa safari ya majaribio ya meli hiyo katika Ziwa Victoria, kueleza kuwa wakati wa majaribio hayo imeendeshwa kwa kasi inayohitajika na kuonesha uwezo wa mkubwa kama inavyohitajika.

Alisema meli hiyo inayogharimu Sh. bilioni 127.27 inatarajiwa kukabidhiwa Mei 31 na baada ya hapo kuanza kazi za majaribio Juni mwaka huu endapo hakutakuwa na kikwazo.

"Tumeanzia kasi ya noti 10 mpaka noti 15 na wakati wote injini na mitambo yote ilikuwa ikifanya kazi vizuri bila tatizo lolote, hivyo kutokana na sisi kuthamini usalama kwanza tunajitahidi kuhakikisha ipo salama ili iweze kuwahudumia Watanzania kama ilivyopangwa," alisema Prof. Mbarawa.

Alisema meli hiyo inatarajiwa kurahisisha shughuli za usafirishaji mizigo pamoja na kupunguza gharama za usafiri katika Ziwa Victoria na kutaja usafirishaji wa majini kuwa chini kulinganisha na usafiri mwingine.

Prof. Mbarawa alisema sasa serikali haitegemei kumuongezea muda wa utekelezaji wa mradi, bali kwa sasa wanashughulikia ukarabati na upanuzi wa miundombinu ya bandari zinazotarajiwa kuhudumiwa na meli hiyo nchini, ikiwemo Bandari ya Kemondo Kagera pamoja na Mwanza Kaskazini.

Mkurugenzi wa Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL), Erick Hamis alisema kukamilika kwa majaribio hayo kunaongeza asilimia tatu katika utekelezaji wa meli hiyo na kufikia asilimia 96.

Alisema asilimia nyingine nne zinazosalia zinahusiana na uwekaji wa samani ndani ambazo ni pamoja na viti, meza, vitanda, kabati, kapeti pamoja na umaliziaji wa kawaida ambako vyote hadi ifikapo Mei 31, mwaka huu vitakuwa tayari.

Meneja Mradi, Luteni Kanali Vitus Mapunda alisema licha ya mradi huo kuelekea kukamilika kwa asilimia 100, utekelezaji wake ulikumbana na changamoto mbalimbali kutokana na meli hiyo kuwa ya kwanza kwa ukubwa kutengenezwa Tanzania na ukanda wa maziwa makuu, hivyo iliwachukua muda kupata mafunzo kadhaa kutoka kwa wahandisi wa Korea.

Nahodha wa meli hiyo wakati wa majaribio Kapt. Bembele Ng'wita alisema katika majaribio hayo ya siku tatu kila kifaa kinachotumika kwenye meli hiyo husani katika mitambo ya uendeshaji kilijaribiwa na kuhakikisha vyote vinafanya kazi katika hali inayohitajika.




Kaimu Ofisa Elimu Wilaya ya Nyang'hwale, mkoani Geita, Jonathan Rwezaula (katikati), akipokea viti na meza zake 160 kutoka kwa Ofisa Uhusiano kwa Jamii wa Mgodi wa Sotta, John Bwana (kulia), kwa ajili ya Shule ya Sekondari Nyamtukuzanhwiga, wilayani Nyang'hwale, mkoani Geita mapema wiki hii. Kushoto ni Diwani wa Kata ya Nyamtukuza, Daudi Mabesa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanafunzi 12 wadaiwa kuchapwa viboko 75 kila mmoja

**Na Elizabeth Seleman,** SENGEREMA

WANAFUNZI 12 wa Shule ya Sekondari Ipandikilo iliyoko Kata ya Ngoma 'B' wilayani Sengerema mkoani Mwanza wanadaiwa kuchapwa viboko 75 kwa kila mmoja.

Hali hiyo imewasababishia kupata majeraha na kulazimika kupatiwa matibabu katika Kituo cha Afya Ngoma 'B'.

Wanafunzi hao wanadaiwa kuchapwa viboko hivyo baada ya kukutwa na makosa ya kinidhamu ikiwemo kujihusisha na mapenzi shuleni kinyume na sheria za shule.

Mkuu wa shule hiyo, John Paulo akielezea tukio hilo juzi alisema wanafunzi hao waliadhibiwa na baadhi ya walimu shuleni hapo na yeye alikuta tayari wameumizwa sehemu mbalimbali za miili.

Alisema alilazimika kuwapeleka katika kituo cha afya ili wakapate matibabu na vipimo wakisaidiana na Mtendaji wa Kata.

Ofisa Mtendaji Kata wa Ngoma 'B', Emili John alithibitisha kupokea taarifa za malalamiko kutoka kwa wazazi na walezi wa wanafunzi hao.

Alisema baada ya kupokea malalamiko hayo alimuuliza Mkuu wa Shule ambaye alimweleza kuwa ilikuwa sehemu ya adhabu ya utovu wa nidhamu na tayari walimu wamechukuliwa hatua ikiwemo kukanywa juu ya kutolewa kwa adhabu za namna hiyo.

Akithibitisha kuwapokea wanafunzi hao, Mganga Mfawidhi wa Kituo cha Afya Ngoma 'B', Abutwale Bukwaje alisema wanafunzi waliopokelewa kituoni hapo ni 12 ambao walibainika kuwa na michubuko katika sehemu mbalimbali za miili yao.

Diwani wa Kata hiyo, Donald Masinde alisema kitendo hicho hakiwezi kuvumiliwa na kukitaja kama sehemu ya ukatili na unyanyasaji kwa wanafunzi, huku akiahidi kuhakikisha wote walihusika wanachukuliwa hatua za kisheria.Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi wilayani Sengerema, Jackson Mazinzi alilaani kitendo cha wanafunzi kuadhibiwa kikatili na walimu hao na kuwataka kuzingatia sheria za utoaji adhabu shuleni.

Hivyo, alimwagiza Mkuu wa Shule hiyo kuwaeleza walimu wake namna sahihi ya kutoa adhabu kwa wanafunzi na siyo kuwachapa viboko visivyo na idadi na kusema suala hilo kuwa kinyume maadili ya ualimu.

# Hospitali ya Wilaya Kahama yakumbwa uhaba wa maji

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAKAZI wa Halmashauri ya Msalala mkoani Shinyanga, wameiomba serikali kupitia Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), kuhakikisha Hospitali ya Wilaya inapata huduma ya maji safi na salama ili kuwaondolea kero wagonjwa na wajawazito

Walitoa ombi hilo juzi wakati wa mkutano wa hadhara wa Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Mboni Mhita uliolenga kusikiliza na kutatua kero za wananchi.

Walisema ni zaidi ya miaka mitatu wamekuwa wakiahidiwa kupata maji kutoka Ziwa Victoria.

Mkazi wa Kijiji cha Ntobo, Marco Makune alisema hospitali hiyo kukosa chanzo cha uhakika cha maji inasababisha adha mbalimbali kwa wajawazito ikiwemo milipuko ya magonjwa.

Alisema kwa sasa hospitali hiyo inategemea kisima kifupi kilichochimbwa na wananchi na kipindi cha kiangazi kinakauka maji hali inayofanya halmashauri kusomba maji kwa kutumia gari la maji.

Stephano Paul alisema licha ya maji kutoka Ziwa Victoria kufika katika kata jirani ya Ngaya vilevile kata hiyo haina maji na wakati wote wamekuwa wakitegemea visima walivyochimba kando ya makazi yao.

Mganga Mkuu wa Hospitali ya Msalala, Dk. Sisti Mosha alikiri kutokuwepo kwa maji ya uhakika.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Mboni Mhita aliwapongeza wananchi kwa kuchimba kisima hicho ili kuhakikisha hospitali inakuwa na maji ya uhakika na kuwa serikali itahakikisha maji ya Victoria yanafika.

Meneja wa RUWASA Kahama, Magili Maduhu alikiri kata nzima kutokuwa na chanzo cha uhakika cha maji na kusema wanatarajia kuchimba kisima kirefu ili kupunguza adha hiyo, huku wakiendelea kusubiri maji ya Ziwa Victoria ambako muda wowote wataanza kulaza mabomba.



Ukurasa 12

**SIKUKUU YA WANAWAKE 2024...**

TAWLAE; kinamama wa kilimo na mazingira watembelea wenzao waliowekeza bustanini




Ukurasa 13

Kunywa maji mpaka Makamu wa Rais atishie kung'oka?



Ukurasa 14

**Miaka mitatu ya Samia na ubora EWURA usimamizi bora ujenzi vituo vya mafuta**


# BUFE

IJUMAA MACHI 29, 2024

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA


DEREVA HONELO RAMADHANI WA BOLT...

# Kutoka enzi teksi yake ya wateja kijiweni, hadi ufanisi mtandaoni

**Na Mwandishi Wetu**

AKIWA na uzoefu wa takribani miaka tisa katika tasnia ya usafiri wa kukodi mtandaoni nchini, Honelo Alli Ramadhani, ana mengi ya kueleza kuhusu tasnia ya uchukuzi wa kidijitali, ambayo ameuona ukikua kutoka miaka ya nyuma hadi sasa.

Huyo baba wa watoto watatu mwenye umri miaka 41, akianzia udereva wa teksi za kawaida. Ameanza kufanya shughuli za kubeba abiria nchini, mwaka 2015. Kwa sasa, anafanya kazi kwenye mtandao wa Bolt Tanzania kama dereva wa gari la kifahari.

Kukodi usafiri mtandaoni, wakati mwingine hujulikana kama 'kukodi gari kwa simu janja'.Ni njia ya usafiri binafsi, ambao abiria humtumia dereva kupitia programu ya simu mkononi kumpeleka mahali halisi.

Ulikuwa wakati wa ujio wa teknolojia hiyo, Honelo alipofikiria kujiunga na kikundi cha madereva, kwani teksi za kawaida zilipotea na abiria wengi kibinafsi walichagua huduma mpya za bei nafuu na uhakika.

Akiwa miongoni mwa madereva wa kwanza kutumia njia mpya ya usafiri binafsi, Honelo akakumbuka jinsi madereva wengi wa magari walipata shida kuendesha mfumo kupitia programu za simu za mkononi.

"Wakati huo, wengi wetu hatukuweza kusoma ramani kama inavyoonyeshwa kwenye simu janja, ili kupata abiria wanaotarajiwa na wakati mwingine, mtandao unaweza kukumbwa na hitilafu ambayo ilisababisha hasara ya mapato," Honelo anaeleza alipohojiwa na gazeti hili.

Hata hivyo, sasa anafuraha programu imeboreshwa, hata kukiwapo hitilafu yoyote, madereva huarifiwa mara moja. Anafafanua: "ikitokea kuharibika kwa mtandao wowote, madereva wanajulishwa na mara nyingi kesi kama hizo hutatuliwa ndani ya muda mfupi sana."

Akizungumzia anavyopata kipato zaidi, mjini Dar es Salaam, kunakosifika kwa kero ya msongamano wa magari, Honela anasema huwa anashauriana na abiria, wakatumia njia za kuunganisha tofauti na barabara kuu.

"Kama dereva wa gari, ni muhimu kushauriana na abiria wako ikiwa unaweza kutumia njia za kuunganisha, ili kuepuka msongamano wa magari katika barabara kuu. Hii huniwezesha kuepuka kuchukua muda mrefu kwenye njia moja na hatimaye kuniwezesha kupata pesa zaidi.

"Pia, ninawauliza kama wanapenda kusikiliza muziki au taarifa za habari kama njia ya kuwafanya wastarehe. Mwanzoni pia, haikuwa rahisi kuwasiliana na abiria wa kigeni kutokana na kikwazo cha lugha, lakini kwa miaka mingi nimejifunza mengi na angalau naweza kuwashirikisha katika mazungumzo madogo," anaieleza.

Honela anatamka kufurahi maisha yake kubadilika tangu kuijikita katika udereva mtandao wa Bolt Tanzania, akiwa katika kiwango cha juu amejipatia gari lake, kupitia mkopo kwake kutoka taasisi ya fedha.

"Sidhani kama ningekuwa katika nafasi ya kununua gari kama dereva wa teksi, lakini shukrani kwa kampuni ya Bolt Tanzania sasa nina miliki gari langu nililolipata kwa njia ya usafiri mtandaoni," anashukuru.



Honelo Alli Ramadhani. **PICHA: MAKTABA**

**MATATIZO YALIYOKO**

Kama ilivyo biashara nyingine, usafiri wa abiria una matatizo yake kama vile abiria wakorofi na walevi, wanaokataa kulipa kiasi kinachohitajika, wanapofika mwisho wa safari zao.

"Lazima utumie hekima unaposhughulika na watu kama hao. Iwapo abiria atakataa kulipa kiasi kinachohitajika, basi nitaripoti kesi kama hiyo kwa Bolt Tanzania, ambao watanirudishia baada ya muda," anaeleza.

Kuhusu usalama unapoendesha gari kwa watu usiowajua, Honelo anasema hana wasiwasi kwa kuwa programu za kuwapokea abiria kwa Bolt hutoa taarifa zote za abiria, kama mahali anakotoka.

"Ukiwa kama dereva, unazungumza na abiria wako kabla hata ya kukutana nao na habari zote na njia zinajulikana kupitia App," anafafanua.

Ili kukabiliana na mahitaji mapya ya abiria, Bolt Tanzania inatuma barua pepe kwa madereva wote kuhusu bidhaa na huduma zote mpya, kama vile ofa za wateja na nyenzo za usalama kwenye App zao.

Anasema, hilo limewafanya madereva waendesha magari, kuwa sawa na maendeleo mapya katika kampuni yake, sasa akitabiri mustakabali mzuri wa huduma za Taxi Mtandao nchini, kwa kuwa abiria wengi wanataka huduma za bei nafuu na za kutegemewa kama zile zinazotolewa na Bolt Tanzania.

"Bolt Tanzania imefanya kazi kubwa ya kutuunganisha na wateja wanaotaka bei nafuu. Ilikuwa ngumu sana kwetu nyakati za zamani, lakini mambo yamerahisishwa kupitia matumizi ya teknolojia," anakiri.

Anawashauri wengine wanaotaka kujiunga na udereva, wasisite kuingia katika tasnia hiyo, akijivuna ni ya uhakika na rahisi, ikiwezesha watu kujihusisha na shughuli nyingi. Katika muda wa ziada asipokuwa kazini, Honelo anasema hutumia kuwa nyumbani akiwa na mke, pia watoto.

Ndoto za Honelo sasa, ananuia kununua kiwanja na kujenga nyumba, kisha akafungua biashara itakayomsaidia uzeeni katika umri hawezi tena kujishughulisha na uendeshaji gari.

UCHUMI

SIKUKUU YA WANAWAKE 2024...

# TAWLAE; kinamama wa kilimo na mazingira watembelea wenzao waliowekeza bustanini

**Na Vidah mahava**

INAPOTAMKWA msamiati TAWLAE, ni kifupi cha msamiati wa Kiingereza, Tanzania Association of Women Leaders in Agriculture and Environment.

Ni taasisi iliyoanzishwa rasmi mwaka 1995, ikiwakusanya wataalamu wanawake katika ufugaji, kilimo na mazingira, ikiwa na matawi mikoa yote ya nchi.

Ndani ya miaka 29 iliyopita, imeongozwa na safu ndefu, ikianza na Mwenyekiti Mama Rhoda Kweka. Badauara akafauatiwa na Mama Ada Mdessa Mwasha; Halima Chande, Dk. Maria Mashingo, Christina Lyimo, kisha Sophia Mlote.

Kwa sasa Mwenyekiti ni Mama Elde Kimaro na Mkurugenzi wa Miradi katika kipindi kirefu amekuwa, Mary Liwa.

Ndani ya safari yake hiyo, TAWLAE imekuwa na mafanikio makubwa katika jukumu lake kuhudumia jamii, ikiwamo kusaidia udhamini wa masomo kwa watu mbalimbali, pia mafunzo ya kilimo, ufugaji na mazingira kwa kinamama, vijana na vikundi.

Hiyo imeendana na kusaidia sana kupunguza utumikishawji wa watoto kwenye mashamba ya wakulima wadogo wa tumbaku. Kilichofanyika sasa, wamehamasisha vijana wa kike na kiume kufanya kazi katika mashamba darasa, ili kujifunza kwamba 'kilimo ni ajira.;

Mjumuiko huo sasa umeanzisha vikoba kwa wanawake, sasa ikipanuka katika sura pana na huduma za benki ya wanawake vijijini, ambayo sasa inawawezesha kukopa na kuongeza mitaji katika vikoba. Hali inayoendelea sasa wanawake wengi wamepiga hatua wako kwenye biashara kupitia mikopo na vikoba walivyoanzisha.

Vilevile, imekuwa mstari wa mbele katika vita kutambua na kukabili unyanyasaji wa kijinsia kwa wanawake wa pembezoni, ikijiweka kwenye utetezi wa masuala ya kijinsia, katika tafsiri pana iliyopo.

### SIKU YA WANAWAKE

Katika kuungana na kimataifa, kusherehekea Siku ya Wanawake Duniani Mwaka 2024 yenye kaulimbiu 'Wekeza katika Wanawake Kuharakisha Maendeleo', TAWLAE mkoa wa Dar es Salaam iliadhimisha kwa namna yake.

Hapo ilifanya ziara kutembelea kikundi kiitwacho cha Kijani Kibichi - Kinyerezi, wilayani Ilala, vilevile kuzuru kwa wakulima wa mboga, Kunduchi mboga Ununio, wilaya Kinondoni.

Ni vikundi vilivyofanyiwa ziara hiyo, kwa kupewa elimu ya kilimo bora cha mboga, pia nao wakaeleza changamoto zao na mafanikio waliyopata kupitia shughuli hizo za kilimo.

Kijani Kibichi ni kikundi chenye wanachama hai wanawake 20, wanaojihusisha na kilimo hai cha mboga za majani, wakiwa na kaulimbiu yenye salamu inayowaongoza "Afya Bora kwa kila Familia na Biashara".



Baadhi ya wanachama wa TAWLAE, katika picha ya pamoja. **PICHA ZOTE. VIDAH MWIHAVA**

> **"Ni vikundi vilivyofanyiwa ziara hiyo, kwa kupewa elimu ya kilimo bora cha mboga, pia nao wakaeleza changamoto zao na mafanikio waliyopata kupitia shughuli hizo za kilimo.**



Mwanachama wa TAWLAE, Dk. Ruth Minja, akigawa mbegu za mboga kwa wanakikundi cha Kijani Kibichi- Kinyerezi Dar es Salaam.

Wanakikundi hao huzalisha mboga zao kwa kutumia teknolojia hai ya kutumia mbolea zisizo na kemikali, pia wakizuia wadudu na magonjwa kwa njia hai. Utaratibu wao katika kuzalisha wanaeleza, hutumia vitunguu swaumu na pilipili kukinga wadudu na magonjwa shambani.

Pia, wanataja kilimo cha kutumia kinachoitwa kitalamau shambani 'greenhouse'. Hapo lengo wanataja ni kutunza mazingira, huku wakiwa na uhakika wa kupata chakula na kipato, hata kipindi cha nje ya msimu wa kilimo.

Katika tukio hilo, mdau Mama Sophia Mlote, akakazia kuwa wanawake wana sifa ya kufanya mambo yaliyoshindikana, ikiwamo kuwa na mazingira mazuri, chakula cha kutosha na kilicho salama.

Anaeleza historia ya kuanzishwa kikundi cha Kijani Kibichi, Mama Mlote anasema elimu aliyoipata nchini Uhispania ndio iliyompa chachu ya kukusanya wanawake pamoja na kuanzisha kikundi hicho kuelimishana na kutekeleza malengo yao.

Hap kunmatajwa kuwapo kutunza familia, kufanya biashara na kuwa na kipato endelevu, yaani 'Mama awe na fedha mfukoni'.

Kwa sasa anasema wana shamba kubwa la ng'ombe wanalofanyia shughuli za kilimo, ila bado wana uhitaji kukamilisha taratibu za usajili wa kikundi chao, hata wakawa na shamba maeneo wanakoishi.

Diwani wa Kinyerezi, Leah Mgitu na Ofisa Kilimo wa Kinyerezi, Helena Ihonde, waliohudhuria tukio hilo walipokea changamoto na kuahidi kuzitatua.

Kukazia hoja hiyo, Diwani huyo akawashauri wana - kikundi kuwa na meza yao katika Soko la Kinyerezi, kuwawezesha kuuza mboga zao na kuweka bango kuonyesha upatikanaji wa mboga zilizozalishwa kwa njia ya kilimo hai.

Wakawaambia, ni namna ya kukuza soko la mboga zinazozalishwa, akiwaambia "hakuna kinachoshindikana na ardhi itapatikana kwa ajili ya kilimo cha mboga mboga cha pamoja kwa kufuata utaratibu."

Ofisa Kilimo akawaribisha wanakikundi cha Kijani Kibichi kufika katika Kituo cha Mafunzo ya kilimo na Mifugo, Pugu Kinyamwezi, wilayani Ilala, kujifunza teknolojia mbali mbali, kama za kilimo cha uyoga, nyanya na mazao mengine, pia kupata la uzalishaji.

Hapo anarejeshja ujumbe pana kuwa serikali ya sasa inayoongozwa na mwanamama Dk.Samia Suluhu Hassan, inatoa kipaumbele kikubwa kwenye kilimo.

Hapo akawajulisha wadau hao, kwamba zipo mbolea ya ruzuku, wakiwaomba wakulima hao wakajiandikishe kwake, ili huduma ya mbolea ruzuku iwafikie.

### DARASA KILIMO

Dk. Ruth Minja, Mwenyekiti wa TAWLAE mkoa wa Dar es Salaam, aliyekuwa Mkuu wa Msafara na mwanachama Violeth Mwaijande, Mtafiti kutoka Kituo cha Utafiti wa Kilimo Mikocheni, walitoa elimu ya kilimo cha mboga kilivyo, kuanzia kitaluni hadi shambani.

Hapo wakajadili aina tano za mbegu bora za mboga, ambazo ni mchicha yenye aina tatu; nyanya chungu na mnavu, aina mpya kila moja. Vyote hivyo baadaye wakavigawa kwa wanakikundi na wadau 29.

Pia, Mtafiti Vidah Mahava, kutoka Kituo cha Utafiti wa Kilimo Mikocheni, Dar es Salaam, na mwanachama wa TAWLAE akawapa elimu ya kilimo cha mazao mchanganyiko.

Hapo akatumia fursa ya eneo lake la kitaalamu na huduma kwenye kilimo cha minazi, inapochanganywa mazao mengine ya muda mrefu kama miembe, michungwa na malimau.

Pia, ni michanganyiko ya muda mfupi kama mboga mboga, mihogo, viazi, mahindi na mananasi.

Sambamba na mbegu bora za mboga, Mama Martina Polepole, mwanachama wa TAWLAE na mmiliki wa kampuni ya Dondwe, aligawa mbegu za karanga miti (chestnuts) na kuelezea namna upandaji, utunzaji na faida za matunda hayo.

Wadau wengi walifurahia elimu hiyo na kuahidi kupanda kwenye mashamba yao, wakatumia ili kuboresha afya zao.

### KIKUNDI CHA UNUNIO

Wakulima wa mboga Ununio Wakulima, eneo la Songambele wengi wao wanalima mazao ya nyanya, bamia, mchicha, mnavu, loshuu, maboga na matembele.

Pia, kukashuhudiwa kuwapo wakulima wachache wanaolima mpunga. Hapo kuna mchanganyiko wa wanawake na wanaume, wakijipatia vipato na mlo kwa ajili ya familia zao.

Walipoulizwa kuhusu umiliki wa ardhi, wakulima hao wakalifafanua kila mmoja huonana na walinzi wa eneo husika na kuomba kutumia sehemu ya eneo kwa ajili ya kilimo.

Mkulima husika hufanya makubaliano na mlinzi wa sehemu hiyo na kufanya shughuli alizoziomba.

Rai yao sasa, wanahitaji eneo rasmi kwa ajili ya kilimo cha bustani. Faida nyingine, wakulima wakaeleza shughuli hizi za kilimo zinawaondolea msongo wa mawazo, zinawapa uwezo wa kujifunza na kuwafundisha wengine wanapotembelea mashamba yao.

Katika sura ya changamoto, wakulima hao wanalalamikia uwapo wa mbolea, mbegu na, viuatilifu feki, ukosefu wa elimu bora ya mboga kwa wakulima na ukosefu wa eneo rasmi la kulima mboga.

Hapo wakapatiwa ufafanuzi wa baadhi ya changamoto hizo, Dk. Ruth Minja na wanachama wengine wa TAWLAE wakieleza umuhimu wa kutumia pembejeo bora za kilimo na kwa njia sahihi, wakisisitiza matumizi ya mbolea ya samadi.

Hiyo wakaitaja inaendana na mzunguko wa mazao, kutotumia miche ya jirani isiyo salama, iliyoathirika na kutofukia mabaki ya nyanya, nyanya chungu kwenye eneo unalotaka kupanda jamii ya nyanya, ili kuzuia madhara ya mnyauko na magonjwa mengine.

Katika kilio cha mbegu, wakulima na wadau waliokuwapo Ununio, wakapewa zawadi ya mbegu bora za mchicha, nyanya chungu na mnavu na walielimishwa uoteshaji wake, jinsi ya kuandaa kitalu na utunzaji mboga hizo. Jumla ya wadau 45 walipatiwa mbegu hizo.

Mtaalamu Mama Sophia Mlote, akaeleza umuhimu wa kupunguza matumizi ya kemikali hasa kwa mboga, akishauri matumizi ya kilimo hai, ili kutunza afya ya mlaji na mazingira yaliyopo.

Akafafaua kwa rai kwamba, ikiwa kila mmoja anampenda mwenzake hatataka kumlisha kemikali kupitia mboga.

### MENEJA KIWANDA

Bwana Mkenda, Meneja wa kiwanda cha Mboji - Mabwepande, akawaonyesha wakulima mbolea ya mboji wanayoitengeneza, faida na upatikanaji wake.

Kiwanda hicho kiko chini ya usimamizi wa Manispaa ya Kinondoni na lengo lake ni kupunguza ombwe la upatikanaji, ubora na gharama za mbolea nchini. Hapo wakulima walivutiwa na teknolojia hiyo na wakapewa mboji kiasi, kwa ajili ya majaribio.

Ofisa Kilimo, Agatha Mushi, akaahidi kuzichukua changamoto zinazohusika na manispaa na kuzipeleka sehemu husika.

Akawaeleza wakulima uwapo wa mbolea ya ruzuku na kuwaomba wajiandikishe kwake, wale ambao hawajaandikishwa

*• **Mwandishi kitaaluma pia ni mtafiti kilimo.***

---

TAFAKURI YA MLALAHOI

# Kunywa maji mpaka Makamu wa Rais atishie kung'oka?






NA JOSEPH KULANGWA
(+255) 713 410008
kulangwasos@gmail.com

MKO nyumbani mmetulia kama familia, ghafla baba anaingia na kupiga kelele huku akijiapiza: "Haki ya Mungu huyo kuku asipopikwa leo familia ikala, nitajinyonga!"

Anamwelekea msichana wa kazi na kumtazama kwa hasira na kurudia kiapo. Mzee anaonekana kumaanisha, kwamba haiwezekani kuku kaletwa na kila kitu kipo kuanzia vyombo, jiko na viungo, lakini kuku asipikwe na akaliwa.

Lazima mtashangaa na kumtazama baba kama yuko sawa au la? Lakini, kumbe baba anataka familia yake ifurahie na pengine alishamwangalia msichana wa kazi na kubaini kuwa ana uzembe fulani hivi katika kutekeleza majukumu yake ya msingi na sasa amechoka kumvumilia.

Nanyi kama wanafamilia, mnajiuliza hivi kwa nini asimtimue tu akatafutwa mwingine kuliko kutaka kuhatarisha maisha yake, sasa baba akijitoa maisha nani mtamtegemea kama familia?

Polepole ili kutaka kuokoa hali, mnamfuata baba na kumwuliza kulikoni mpaka aamue kuchukua hatua nzito na ya hatari kama hivi, anakwambieni si mara ya kwanza kuleta vitu nyumbani lakini havishughulikiwi kama anavyotaka.

Msichana wa kazi anaona hatari mbele yake na anajitokeza na kumhakikisha baba, kuwa hakuna litakaloharibika, kwani kuku atapikwa na familia itafurahia kama anavyotaka na kama inavyotakiwa.

Pande zote zinakubaliana na kubaki sasa kufuatilia kitakachofanyika kwa msichana wa kazi, ama kumpika kuku yule au kufukuzwa yeye ili kuokoa maisha ya nguzo ya familia na kuchelea kuitikisa familia.

Simulizi hii inakuja baada ya kumsikia hivi karibuni Makamu wa Rais, Dk Phillip Mpango akiwa kijijini Kiria, wilayani Mwanga, mkoani Kilimanjaro, akifuatilia mradi mkubwa wa maji wa Mwanga/Same/Korogwe.

Maana yake huko anakuta madudu, anapoona mradi huo wenye thamani ya Dola za Marekani milioni 300 unaofadhiliwa na serikali pamoja na mashirika ya misaada ya Umoja wa Falme za Kiarabu, ukisuasua.

Kwa kulitambua hilo lakini na uzito wa ahadi za Rais Samia Suluhu Hassan kwa wananchi wa maeneo hayo wenye kero sugu ya maji, Dk Mpango anaamua kujitoa mhanga na kuweka rehani wadhifa wake.

Anasema, yuko tayari kujiuzulu wadhifa wake endapo mradi huo unaohudumia watu 438,000 utakuwa haujakamilika ifikapo Juni mwaka huu.

"Sina uso wa kuja kutazama wananchi walioahidiwa maji kwa miaka 19 sasa... nitajiuzulu, ila sijui kitatokea nini kwa walio chini yangu...!" anatamka.

Sasa basi, ili mradi huo ukidhi mahitaji ya watu hao kisawasawa ni mpaka mwaka 2038, yaani miaka 14 ijayo! Nampa pole sana kiongozi wangu huyu kwa kuonyesha ni jinsi gani anaumizwa na matatizo ya wananchi wa maeneo hayo.

Lakini labda turudi kwenye matatizo ya jumla ya maji katika nchi hii iliyopata uhuru mwaka 1961, nchi ya Maziwa Makuu, ikiwa imezungukwa na maziwa matatu makubwa Afrika, achilia mbali Bahari ya Hindi, mito, vijito na mabwawa.

Watanzania sijui tulijikwaa wapi, kwa sababu miaka ya awali ya uhuru, maji yalikuwa ya kumwaga, yakipatikana mijini tena kwa kuingiza sarafu ya chapa kwenye bomba na maji kutoka, lakini leo tumerudi kuchimba visima vilivyotumiwa na mababu zetu.

Tungekuwa makini katika majukumu yetu, na kama wizara za maji zilizokuwapo tangu uhuru, zingefanya kweli majukumu yao kwa maslahi ya Taifa na si ya viongozi, tusingekuwa na haja ya Wizara ya Maji leo, kwani maji yangekuwapo bila hata kusimamiwa.

Ngoja tusubiri, tukiona kwa wa Mwanga, Same na Korogwe mwaka 2038 maji yanapatikana bila matatizo kutokana na tishio la Makamu wa Rais kuachia ngazi, basi Makamu atakeyakuwapo wakati huo, naye atishie hivyo mwaka huo, ili Tanzania iwe na maji ya uhakika kila kona. Kazi iendelee!

UCHUMI

# Miaka mitatu ya Samia na ubora EWURA usimamizi bora ujenzi vituo vya mafuta

**Na Mwandishi Wetu**

MIAKA mitatu ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan madarakani imeendelea kuwa mfano wa kuigwa kutokana na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) kuwa taasisi imara na mfano.

Hali hiyo inatokana na mamlaka kuendelea kusimamia ubora wa ujenzi wa vituo vya mafuta na kuhakikisha upatikanaji wa bidhaa za mafuta katika maeneo yote nchini.

Akizungumza katika mahojiano maalum, Meneja Mawasiliano na Uhusiano wa EWURA, Titus Kaguo, alisema hadi Februari, mwaka huu, kulikuwa na vituo vya mafuta 2,458 vyenye leseni. Kati ya vituo hivyo, vilivyoko mijini ni 2,058 na vijijini zaidi ya 400.

"Serikali imeendelea kuhamasisha na kusimamia ujenzi wa vituo vya mafuta katika maeneo ya mijini, lakini pia kwa vijijini kumekuwa na hamasa kubwa baada ya EWURA kulegeza masharti ya ujenzi wa vituo vya mafuta vyenye gharama nafuu vijijini. Lengo likiwa ni kurahisisha upatikanaji wa bidhaa za mafuta zenye ubora na kuuza katika hali ya usalama katika maeneo mbalimbali." alisema

Pia alisema EWURA imeendelea kusimamia ubora wa vilainishi vinavyoingizwa katika soko hapa nchini kwa kutoa leseni kwa wafanyabiashara wanaofanya biashara ya jumla ya vilainishi.

"Mamlaka imetoa zaidi ya leseni 70 za biashara ya jumla ya vilainishi na leseni saba za viwanda vya kutengeneza bidhaa hizo. EWURA imekuwa ikishirikiana na taasisi zingine za serikali.

"Kwa mujibu wa Kanuni ya 56 (1) ya Kanuni za Petroli (Shughuli za Vilainishi) 2022, Gazeti la Serikali Na. 115 la tarehe 4/3/2022, mfanyabiashara atakayekutwa na vilainishi visivyokidhi viwango atachukuliwa hatua za kisheria ikiwemo kutozwa faini isiyopungua Sh. milioni 10 kwa anayezalisha vilainishi, Sh. milioni saba kwa muuzaji wa jumla, Sh. milioni sita kwa msambazaji; na Sh. milioni tano kwa muuzaji wa rejareja. Adhabu hizo zinaweza kuambatana na vifungo mbalimbali kwa mujibu wa sheria," alisema.

Katika kusimamia ubora wa vilainishi, alisema EWURA kwa kushirikiana na Tume ya Ushindani (FCC) na Shirika la Viwango Tanzania (TBS) hufanya ukaguzi kubaini bidhaa za vilainishi zilizoko sokoni ambazo hazikidhi viwango vya ubora stahiki na kuchukua hatua kwa mujibu wa sheria.



Mkurugenzi Mkuu wa EWURA, Dk. James Andilile (kulia) akimkabidhi kibali cha ujenzi Meneja Mkuu wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) Tanzania, Wendy Brown. EWURA inasimamia EACOP katika masuala ya kiufundi na ushirikishwaji wa Watanzania katika mradi huo. **PICHA: EWURA**

> **Katika kipindi hicho pekee, EWURA imetoa leseni 1021 kwa makandarasi wa umeme (electrical installations personnel) kwa madaraja mbalimbali.**

Pia alisema kutokana na matokeo ya ukaguzi huo, EWURA imeanzisha kampeni ya ukaguzi kwa mikoa yote nchini ili kudhibiti tatizo hilo ambalo limekuwa na athari kubwa kwa wananchi.

### PROGRAMU UWEKAJI VINASABA

Meneja huyo alisema EWURA inaendelea kutekeleza programu ya uwekaji vinasaba katika mafuta na kuhakikisha mafuta yanayouzwa hapa nchini yamelipiwa kodi stahiki na pia kudhibiti ubora.

"Katika programu hiyo TBS ina jukumu la kuweka vinasaba katika mafuta yote yanayotumika hapa nchini ambayo yamelipiwa kodi na EWURA ina wajibu wa kufanya ukaguzi katika soko la ndani kuhakikisha mafuta yanayouzwa nchini yamezingatia kiwango stahiki cha vinasaba," alisema na kuongeza kuwa matumizi ya mafuta yote hapa nchini yaliyolipiwa kodi ni takribani lita 12,000,000 kwa siku.

Pia alisema katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Februari, mwaka huu, mamlaka imeendelea kutekeleza shughuli mbalimbali za udhibiti wa sekta ya nishati ikiwamo kufanya ukaguzi wa miundombinu ya usambazaji umeme. Lengo ni kutathmini ubora wa miundombinu hiyo ili kuhakikisha upatikanaji wa uhakika wa umeme kwa wananchi.

"Katika kipindi hicho pekee, EWURA imetoa leseni 1021 kwa makandarasi wa umeme (electrical installations personnel) kwa madaraja mbalimbali", alisema.

"EWURA pia imeendelea kutoa leseni kwa kuchakata maombi ya leseni za umeme, mafuta na vibali vya ujenzi wa miundombinu ya mafuta kupitia mfumo wa mtandao (Licensing and Order Information System – LOIS)" alisema.

### AKIBA YA MAFUTA

Kaguo alisema mamlaka imeendelea kuhakikisha wakati wote nchi ina mafuta ya kutosha kukidhi mahitaji kwa kusimamia mfumo wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (BPS) na kuhakikisha Kampuni za mafuta zina mafuta ya kutosha kwa kufuatilia akiba ya mafuta ya kila lampuni kila mwisho wa wiki.

Kuhusu mfumo wa taarifa wa mafuta na gesi (NPGIS), Kaguo alisema unaiwezesha EWURA kupata taarifa za hali ya upatikanaji wa mafuta nchini, alisema mfumo huo umefanikisha upatikanaji wa taarifa sahihi za mafuta na gesi hivyo kurahisisha utekelezaji wa masuala ya kiudhibiti.

Katika sekta kudhibiti sekta ndogo ya gesi asilia, alisema mamlaka hufanya ukaguzi wa mara kwa mara katika miundombinu ya uchakataji, usafirishaji na usambazaji wa gesi asilia katika mikoa ya Mtwara, Lindi, Pwani na Dar es Salaam.

### UWEKEZAJI CNG

Aidha, alisema EWURA imewashauri wawekezaji kuwekeza kwenye vituo vya gesi asilia iyogandamizwa (CNG) kwani soko bado ni kubwa ikilinganishwa na vituo vya mafuta.

EWURA imesema changamoto zinazoikabili sekta hiyo ikiwamo uwekezaji mdogo katika usambazaji wa nishati hiyo ya kuendesha magari, viwanda na matumizi ya nyumbani na shughuli nyingine za uzalishaji zitakwisha iwapo wananchi wenye uwezo watatumia fursa zilizopo kwenye sekta kuwekeza.

Kaguo alisema hivi karibuni kuwa tayari serikali imeandaa kanuni za uendeshaji wa CNG zinazosimamiwa na EWURA, lakini tatizo bado ni mwamko mdogo wa uwekezaji, hivyo EWURA kwa kushirikiana na wadau wengine inaimarisha kampeni za uhamasishaji, ili kuvutia wawekezaji.

"Serikali imeweka mazingira wezeshi, na tunachukua hatua madhubuti kuhakikisha uwekezaji kwenye CNG unashamiri ili tuimarishe upatikanaji wa huduma na kurahisisha maisha ya Watanzania," alisema Kaguo.

Baadhi ya wadau wa ngazi ya serikali wanaohusika kutoa suluhu ya changamoto zinazokabili mnyororo wa uwekezaji kwenye CNG wakiwamo Wizara za Fedha, Nishati na Ardhi, Mamlaka ya Mapato Tanzania (Tra) , Baraza la Usimamizi wa Mazingira (nemc), Shirika la Viwango na Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT), watakutana hivi karibuni katika kongamano la kujadili changamoto na namna ya kuipeleka mbele sekta ya gesi asilia.

Alisema fursa za uwekezaji katika CNG ni pamoja na kituo mtandao (matumizi ya umma/ au ya kibinafsi); kituo cha kujaza CNG nje ya mtandao (matumizi ya umma/ binafsi); kituo dada cha CNG (kwa matumizi ya viwanda, biashara, uzalishaji wa umeme au katika kaya); usafirishaji wa CNG; karakana za kubadili mifumo ya magari kuweza kutumia CNG; wahakiki/wakaguzi wa mifumo ya CNG na magari yaliyobadilishwa mfumo (teksi, mabasi na malori).

Kwa sasa, alisema kuna vituo vitano vinavyotoa huduma ya gesi asilia iliyokandamizwa kwenye magari, taasisi saba zinazotumia CNG, zaidi ya viwanda 30, nyumba 1,552, vituo 10 vya kubadilisha mifumo ya magari na magari 3,758 yaliyobadili mfumo ili kutumia CNG katika mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Lindi na Mtwara.

Alisema EWURA hutoa vibali vya ujenzi wa miundombinu ya CNG ndani ya siku 30 na leseni za uendeshaji ndani ya siku 60 baada ya kupokea maombi kamili. Gharama za kibali cha ujenzi, alisema ni Sh. milioni tano na leseni Sh. 1,500,000 ambayo hudumu kwa miaka isiyopungua 25.

# Watoa mapendekezo kudhibiti magonjwa yasiyoambukiza

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WADAU wa mkutano wa kwanza wa kimataifa wa afya ya msingi wametoa mapendekezo kwa serikali na kutiliwa mkazo elimu ya kujikinga na magonjwa yasiyo ya kuambukiza ambayo kwa sasa ni tishio kwa jamii.

Akisoma mapendekezo hayo wakati wa kufunga mkutano huo, Prof. Bruno Sunguya kutoka Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS), alisema magonjwa hayo yanaongezeka na kuwa mzigo mkubwa kwa serikali.

"Ni muhimu ngazi ya jamii kupambana na visababishi na kuhakikisha ngazi ya afya ya msingi wagonjwa watambuliwe na kuhudumiwa mapema ili kupunguza mzigo kwa serikali, elimu ya kujikinga na maambukizi ifanyike, tubuni namna mbalimbali za kusaidia."

"Wahudumu wa afya ngazi ya jamii ni muhimu sana kusaidia hili hasa katika hatua za kujikinga na magonjwa yasiyo ya kuambukiza," alisema.

Aidha, alisema wameshauri katika uandaaji wa bajeti za masuala ya afya uzingatie masuala ya msamaha wa matibabu katika utekelezaji wa sera ya afya kwa wote.

Katika eneo la utawala, alisema wadau wameshauri kuongezwa kwa mafunzo ya uongozi na utawala kupitia mitaala ya kiuongozi.

Kuhusu dawa na vifaa, alisema kuna tatizo katika eneo la ugavi na hivyo kuna haja ya kuboresha upatikanaji wa vifaa tiba na vitendea kazi ili kuboresha utoaji huduma ngazi ya chini.

Akizungumzia suala la rasilimali watu, alisema wadau wametoa mapendekezo ya kuboreshwa kwa mitaala kwenye vyuo ili kuendana na mahitaji yaliyopo.

Alisema pamoja na jitihada za kupunguza vifo vya mama na mtoto lakini bado takwimu si stahimilivu na ni eneo linalohitaji kuboreshwa kwenye ubora wa utoaji huduma.

Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais TAMISEMI anayeshughulikia Afya, Dk. Wilson Mahera alisema wadau wamejadili kwa kina upatikanaji wa fedha za kutosha kwa huduma za afya ya msingi.

Alisema: "Mapendekezo mengine ni kuongeza bajeti za afya za mifumo ya bima na jambo hili limesisitizwa kwa ukubwa na wakashauri vyanzo mbalimbali viweze kutumika ikiwemo kuwashirikisha wadau kama Wizara ya Fedha".

Akifunga mkutano huo, Naibu Waziri wa Afya, Dk.Godwin Mollel, alikemea urasimu wa usajili wa vituo binafsi vya afya.

Aidha, aliwaonya washitiri ambao wamekuwa wakikwamisha upatikanaji wa dawa kwenye vituo vilivyoingia nao mkataba.




Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel (kulia), akimsikiliza Mkurugenzi wa Ubunifu wa Afya wa Taasisi ya PharmAccess, Zamaradi Mbega (wa pili kushoto), wakati alipotembelea banda la taasisi hiyo, wakati wa mkutano wa kimataifa wa afya ya msingi kuhusu ugharamikiaji wa huduma za afya ya uzazi kwenye Bima ya Afya kwa Wote (UHI), jijini Dodoma hivi karibuni. **ICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kiwango unywaji maziwa chashuka, ushauri watolewa

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

IMEELEZWA kuwa wastani wa unywaji wa maziwa hapa nchini ni lita 62 kwa mtu mmoja, huku kiwango kinachotakiwa ni lita 200 kwa mwaka.

Kutokana na hilo, wachakataji wa maziwa nchini wameshauri kuanzishwa vituo maalumu vya kuuza maziwa (ATM) ili kuwasogezea wananchi huduma hiyo.

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Prof. Daniel Mushi aliyasema hayo wakati wa kukabidhi vibanda vya kuuzia maziwa kwa baadhi ya shule hapa nchini.

Prof. Mushi alisema unywaji wa maziwa hapa nchini bado upo chini, hivyo zinatakiwa juhudi zaidi za kuwahamasisha watu kupenda kutumia chakula hicho.

Kadhalika, aliwataka wachakataji hao kuhakikisha kuwa ATM hizo zinakuwa na uwezo wa kuuza maziwa kuanzia gharama chini ili watu wa kila hali wananunua.

Kadhalika aliwataka wachakataji hao kuongeza bei za kununua maziwa kwa wafugaji wengine ili kuwasaidia kuinua uchumi wa kundi hilo ambalo halifaidiki na zao hilo.

Alisema kuna malalamiko kwa baadhi ya wafugaji kudai kuwa hawapati bei nzuri wakiuza kwa wenye viwanda vya kuchakata, hivyo aliwataka kulifanyia kazi jambo hilo.

Msajili wa Bodi ya Maziwa Tanzania, Prof.George Msalya alisema katika kuhamasisha Watanzania kupenda kunywa maziwa wameanza na kutoa vibanda nane kwa ajili baadhi ya shule hapa nchini.

Prof Msalya alizitaja shule hizo zilizokabidhiwa vibanda hivyo vya kuuzia maziwa kuwa ni Shule za Msingi Ilazo na Mlezi za Mkoa wa Dodoma, Shule za Msingi Majnje ,Mwenge ,Jagro na sekondari ya Mshikamano zote za mkoani Mbeya na Mkoa wa Morogoro ni shule za msingi za Michikichini B na Mafiga B.

# Serikali yakamilisha ujenzi wa Shule Miyuji B

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WANAFUNZI wa Shule ya Sekondari wa Miyuji B mkoani hapa waliokuwa wanatembea zaidi ya kilometa saba kufuata elimu katika Kata ya Mnadani, wameondokana na adhaa hiyo baada ya serikali kuwajengea shule.

Mwakilishi wa Mkuu wa Idara ya Elimu Sekondari, Fredrick Mwakisambwe aliyasema hayo alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari waliotembelea shule hiyo ili kuona mafanikio ya miaka mitatu ya Rais Samia Suluhu Hassan.

Mwakisambwe alisema serikali imejenga Shule ya Sekondari Miyuji B hatua ambayo imewasaidia wanafunzi waliokuwa wakitembelea umbali mrefu kufuata elimu katika Kata ya Mnadani.

Alisema kuwa shule hiyo imekamilika na imeanza kupokea wanafunzi wa kidato cha kwanza.

Alisema watoto hao walikuwa wakiteseka kwa muda mrefu kutembea umbali mrefu kufuata huduma ya elimu, hali ambayo ilikuwa ikisababisha baadhi yao kuacha shule na wasichana kupata mimba.

"Tunamshukuru Rais Samia, mwaka jana alitupatia Sh.milioni 544 kwa ajili ya kujenga shule hii ya kisasa kabisa yenye madarasa nane, maabara tatu, jengo la utawala, jengo la Tehama na matundu ya vyoo," alisema.

Mkuu wa shule hiyo, Clara Mwinshehe alisema kuwapo kwa shule hiyo itakuwa ni ukombozi kwa wanafunzi hasa wakike ambao walikuwa wanashindwa kumaliza masomo.

# UWT, China 'kimeeleweka' uwekezaji nishati safi ya kupikia

**Na Mwandishi Wetu**

KATIBU Mkuu wa Umoja wa Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi (UWT), Jokate Mwegelo, amewakaribisha wawekezaji kutoka China kuja kuwekeza katika nishati safi ya kupikia, ili kuwasaidia wanawake. Pia ametaja fursa za uwekezaji zinazopatikana ndani ya UWT ikiwemo mpango wa kuanza kuzalisha mkaa mbadala.

Alitaja fursa hizo jana alipotembelewa na ujumbe wa wafanyabiashara kutoka jimbo la Changzhou nchini China, uliotembelea ofisi za CCM kwa ajili ya kuangalia fursa za uwekezaji.

Alisema pamoja na fursa hiyo katika eneo la nishati safi ya kupikia, pia UWT inahitaji uwekezaji katika maeneo ya kilimo na nishati ambako wanawake wengi wanafanya shughuli zao kila siku.

Jakate pia aliwakaribisha wawekezaji hao kuja kuwekeza katika sekta ya madini hususani kuwasaidia wanawake wanaojishughulisha na uchimbaji.

Aidha, alisema UWT pia inahitaji uwekezaji katika eneo la kilimo ambalo wanawake wengi wamejikita, jambo ambalo pia limeonekana kuwavutia wawekezaji hao hususani uzalishaji wa parachichi ambalo lina mahitaji makubwa katika jimbo la Changzhou. Mhandisi kutoka Kampuni ya Canopus Energy Solution, Anna Nyangasi alisema ujio wa ujumbe huo ni fursa kwa uwekezaji katika sekta mbalimbali.

Anna alieleza kuwa wawekezaji hao waliongozwa na Shen Don kutoka Jimbo la Shangzhou ambapo ukiwa nchini ulikutana na wadau mbalimbali kabla ya jana kukamilisha ziara yao kwa kukutana na UWT. Alisema wawekezaji hao wameridhia kufanya uwekezaji wa zaidi ya Dola za Marekani milioni 312 katika maeneo ya nishati, afya, ujenzi, kilimo na vifaa vya uchakataji.

Pia, alisema ujumbe huo umeonesha nia kushirikiana na kutafuta wawekezaji katika maeneo takribani manane ambayo ni viwanda vya kuonganisha zana za kilimo, kuzalisha vifaa vya trekta, majenereta, pampu za maji, vifaa tiba, viwanda vya bidhaa za umeme na 'paneli' za kuhifadhi baridi.





# Madereva malori, abiria, viongozi wapigwa msasa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MADEREVA wa magari ya mizigo, abiria na viongozi wametakiwa kuzingatia sheria, alama na michoro ya usalama barabarani ili kuepuka ajali ambazo zimekuwa zikigharimu maisha ya watu na kuharibu mali.

Kauli hiyo ilitolewa juzi na Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi, Benjamin Kuzaga wakati akifungua mafunzo kwa madereva wa magari ya mizigo, abiria na viongozi.

Mafunzo hayo yalifanyika katika Chuo cha Udereva cha Agility Professional Driving School (APDS) cha jijini Mbeya ambacho ni miongoni mwa vyuo vilivyoteuliwa kutoa mafunzo hayo.

Kamanda Kuzaga aliwataka madereva kuheshimu watumiaji wengine wa barabara kwa maelezo kuwa nao wana haki ya kutumia barabara kwa mujibu wa sheria.

"Mbali ya vyombo vya moto kuna watumiaji wengine wa barabara, wapo watu wenye ulemavu, watoto, watu wenye uoni hafifu na viziwi, hao nao wana haki ya kutumia barabara, waheshimuni kwa kuhakikisha mnafuata sheria," alisema Kamanda Kuzaga.

Alisema maeneo yote ambayo watu wanavuka zimewekwa alama ambazo zinaashiria kuwa wanatakiwa kupunguza mwendo ama kusimama ili kuruhusu watu hao kuvuka.

Hata hivyo alisema mbali na alama za usalama barabarani lakini pia wapo askari wa usalama barabarani ambao wanakuwa wanatoa ishara mbalimbali kwa madereva.

Mkufunzi wa udereva, David Mtunguja kutoka Chuo cha Ufundi Arusha aliwasisitiza kuhakikisha wanapoendesha wahakikishe wanayafahamu vizuri magari yao ili kubaini kama kuna hitilafu ya aina yoyote na kuchukua hatua.

Mkurugenzi wa Agility Professional Driving School, Anthony Malamla aliomba Serikali kuongeza nguvu ya udhibiti wa vyuo vya udereva ambavyo havijakidhi vigezo wala kusajiliwa, ili kuepuka utapeli na kuzalisha madereva wasio na weledi katika taaluma ya udereva.

# Utafiti: Asilimia 76 ya watu wazima wameoza meno

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

UTAFITI wa afya ya kinywa na meno uliofanyika nchini umebaini kuwa asilimia 76 ya watu wazima wameoza meno, huku asilimia 67 wakiwa wanasumbuliwa na matatizo ya fizi.

Mkurugenzi Msaidizi wa Afya ya Kinywa na Meno wa Wizara ya Afya, Dk. Baraka Nzobo aliyasema hayo juzi jijini Mbeya wakati wa kutoa elimu kwa wauguzi wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya kuhusu umuhimu wa afya ya kinywa na meno kwa wajawazito.

Alisema utafiti huo ulifanywa na Wizara ya Afya na kwamba matatizo hayo ya kinywa na meno yanawaathiri zaidi wanawake wajawazito kwa kuwasababishia kifafa cha mimba, kujifungua watoto njiti na mimba kuharibika.

Alisema kutokana na madhara hayo wameamua kuanzisha kampeni maalumu ya kuhamasisha wataalamu wa afya hasa wauguzi kuwasaidia wajawazito kuepuka madhara ya matatizo hayo ya afya ya kinywa na meno.

"Lakini pia utafiti huo umebaini kuwa asilimia 67 ya watu wazima wanasumbuliwa na matatizo ya fizi, asilimia 58 ya watoto wanasumbuliwa na matatizo ya fizi na asilimia 33.1 ya watoto wameoza meno, kwahiyo tatizo hili ni kubwa na lazima tuchukuwe hatua," alisema Dk. Nzobo.

Alisema ili kukabiliana na tatizo hilo wananchi wanatakiwa kuchukua tahadhari kwa kupiga mswaki mara kwa mara hasa asubuhi baada ya kunywa chai na usiku kabla ya kulala pamoja na kutembelea kiliniki za kinywa na meno kwenda kufanya uchunguzi.

Mratibu wa Afya ya Kinywa na Meno wa Mkoa wa Mbeya, Dk. Maisara Karume alisema waliamua kuendesha mafunzo hayo kwa wauguzi ili wawatambue mapema wajawazito wenye matatizo ya kinywa na meno na kuwasaidia.

Alisema wakishawatambua wanatakiwa kuwasaidia mbinu za kufanya usafi ili waepuke madhara yanayoweza kuwakuta ikiwemo kuzaa watoto wenye uzito pungufu na madhara mengine yanayosababishwa na matatizo ya afya hiyo.

Alisema wakati wajawazito watakapokuwa wanahudhuria kliniki moja kati ya vitu watakuwa wanapimwa ni pamoja na afya ya kinywa na meno pamoja na kuwaelimisha kuhusu kuwasaidia watoto wao kuepuka matatizo ya kinywa na meno.

"Hii itawasaidia wataalam wenzetu hawa kutoa huduma kwa kina mama zetu wajawazito wanaokwenda kuhudhuria kiliniki ili kuwaepusha na madhara hayo ambayo yamebainika kuwa yanaathiri afya zao na za watoto wao," alisema Dk. Karume.

Daktari wa meno kutoka mkoani Morogoro, Dk. Calorine Sakaya alisema wanawake wakishapata mafunzo hayo itakuwa rahisi elimu hiyo kusambaa kwa wananchi wengine na kupunguza matatizo ya kinywa na meno.

Alisema wanawake ni rahisi hata kuwaelimisha watoto wao na kuwasimamia wanapofanya usafi wa kinywa kwa kuhakikisha hatua zote muhimu zinafuatwa.

Baadhi ya wauguzi walioshiriki mafunzo hayo, walikiri kuwa awali walikuwa hawajui kama afya ya kinywa na meno ina uhusiano na matatizo ya uzazi kwa wajawazito.

Muuguzi wa Zahanati ya Isyesye jijini Mbeya, Grace Kihai alisema kabla ya mafunzo hayo alikuwa anajua kwamba mjamzito akisumbuliwa na jino hatakiwi kung'olewa mpaka atakapojifungua jambo ambalo baada ya mafunzo alibaini kwamba siyo kweli.



Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, SACP Benjamin Kuzaga (wa tatu kushoto), akisikiliza maelezo ya mchoro wa kufundishia madereva kutoka kwa Mkurugenzi wa Shule ya Udereva ya Agility Professional, Anthony Malamla (kulia), kabla ya kufungua mafunzo ya usalama barabarani kwa madereva, jijini Mbeya juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Mume atuhumiwa kumuua mkewe kisa kuchelewa kurudi

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

JESHI la Polisi Mkoa wa Njombe linamshikilia, Robert Chagavali (33) mkazi wa Kijiji cha Kichiwa kilichopo Wilaya ya Njombe kwa tuhuma za kumuua mke wake, Nuru Mkula (32) chanzo kikitajwa ni kuchelewa kurudi nyumbani.

Kamanda wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Njombe, Kamishna Msaidizi Mahamoud Banga alitoa taarifa hiyo wakati akizungumza na waandishi wa habari mkoani hapa.

Alisema Nuru Machi 22 mwaka huu majira ya saa nne asubuhi alikuwa na ugomvi na mume wake, chanzo kikitajwa ni alitoka kwenye mashamba ambayo alikuwa anavuna ulanzi na kwenda kutafuta dawa lakini alichelewa kurudi nyumbani.

Alisema mnamo Machi 23 mwaka huu kulitokea kutoelewana tena na kuanza kugombana lakini baadae ikaripotiwa tukio kuwa mwanamke huyo amefariki.

"Kwahiyo Jeshi la Polisi tulifika eneo la tukio kwa ajili ya kukagua lakini tuliona kama kuna dalili kuwa na alama za miguu mingi kama kunawezekana kulikuwa na ugomvi kati ya hawa wawili," alisema Banga.

Kamanda Banga alisema baada ya mwili wa marehemu kufikishwa Kituo cha Afya Makambako na kufanyiwa uchunguzi na daktari ilionekana shingo ya marehemu ilikuwa imenyongwa.

Alisema baada ya taarifa hiyo inaonekana wazi kuwa aliyefanya tukio hilo ni mume wake ambaye jeshi hilo linamshikilia katika Kituo cha Polisi Makambako na taratibu zingine zinaendelea za kimashtaka dhidi ya mtuhumiwa huyo.

Alisema mtuhumiwa huyo anavyoonekana ni mtumiaji wa pombe za kienyeji na inaonekana kuwa siku ya tukio alitumia kilevi ingawa hawakumpima na shughuli zake ni kugema ulanzi na kuuza.

Kutokana na tukio hilo, Kamanda Banga aliwataka wananchi mkoani Njombe kupunguza unywaji wa pombe ya ulanzi akisema kiafya siyo nzuri na inaweza kukusababishia kufanya vitendo vya kikatili.

Mtendaji wa Kijiji cha Mji Mwema, Maneno Mguta alisema marehemu na mume wake wote walikuwa watumiaji wa pombe ya ulanzi na siku ya tukio walikuwa wamelewa.

Baadhi ya wakazi wa Njombe Mjini akiwemo Marygoreth Richard alilaani tukio hilo la kikatili na kuiomba serikali kuendelea kutoa elimu itakayosaidia kupunguza vitendo vya kikatili.



# Dk. Mwinyi: Tumeweka mazingira rafiki kukuza sekta ya fedha

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi amesema Serikali itaendelea kuweka mazingira rafiki na wezeshi ya kiuchumi ili kukuza sekta ya fedha nchini.

Aliyasema hayo jana visiwani hapa, katika hotuba yake iliyosomwa kwa niaba yake na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdalla wakati wa uzinduzi wa Ripoti ya Utafiti Finscope Tanzania 2023 kwa upande wa Zanzibar.

Dk. Mwinyi alisema kuwa serikali itaendelea kuweka mazingira rafiki ya kiuchumi ikiwemo kuunda sera zinazozingatia mahitaji ya sekta, kuweka mfumo na kanuni wezeshi za udhibiti pamoja na kushirikiana kwa karibu na wadau wote wa sekta ya fedha, ili kushughulikia changamoto zinazokwamisha mafanikio kwenye utendaji.

Alisema kuwa wakati Serikali ikiendelea kuweka mikakati jumuishi pamoja na kuboresha miundombinu ya msingi, FSDT ina wajibu wa kupanua wigo wa huduma za kifedha, kusaidia ukuwaji wa kampuni na sekta binafsi pamoja na kuchangia ukuwaji wa uchumi na maendeleo ya nchi.

Aidha alisema Ripoti ya FinScope itasaidia katika kubuni mbinu zitakazotumika katika utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Zanzibar (2023-2050), Mpango Mkakati wa Taifa wa Huduma Jumuishi za Fedha (2023- 2028) na mipango mengine ya kimaendeleo pamoja na kutatua changamoto zilizopo.

Hata hivyo alisema Serikali ya Zanzibar imejipanga kuhakikisha kuwa maendeleo ya sekta ya fedha na hali ya huduma jumuishi za fedha nchini zinaimarika.

Dk. Mwinyi alisema bado kuna kazi kubwa ya kuhakikisha Wazanzibar wenye umri wa kufanya kazi, hususani wanawake wanafanikiwa kupata kipato binafsi ili kupunguza utegemezi na kuongeza matumizi ya bidhaa na huduma mbalimbali za fedha.

Hivyo aliwataka wadau wa sekta ya fedha kuendelea kuunga mkono jitihada za Serikali za kuboresha hali ya huduma jumuishi za kifedha kama zilivyoainishwa katika Dira ya Maendeleo ya Zanzibar.

Pia aliwahakikisha kuwa serikali iko tayari kushirikiana na wadau wa maendeleo nchini kwa lengo la kukabiliana na vikwazo vya maendeleo katika sekta ya fedha kwa kuzingatia sera, kanuni na miongozo ya nchi.

Naye Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, Dk. Saada Mkuya Salum, alisema bado kuna matumizi finyu ya bima ya afya nchini, hivyo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeona umuhimu wa kuanzisha Mfuko wa Bima ya Afya Zanzibar.

Kadhalika aliyataka mabenki kutafuta utaratibu mwengine wa kufungua huduma za fedha kwa jamii ili kurahisisha upatikanaji wa kuweka fedha benki kwa urahisi na kupunguza gharama.

Dk. Mkuya alisema katika kutekeleza hilo kuna haja ya kusambaza matokeo ya utafiti huo kupitia njia sahihi ili kuhakikisha kunafanyika maamuzi na kubuni bidhaa na huduma zinazopatikana kirahisi kwa gharama nafuu na kuzingatia mapendekezo na matakwa ya watumiaji ili kuwafikia watu wengi zaidi.

Kaimu Mkurugenzi wa Mfuko wa Kuendeleza Sekta ya Fedha Tanzania, Erick Masinde alisema ripoti hiyo imekuwa na lengo la kuikuza sekta ya fedha na kuimarisha upatikanaji wa huduma za fedha ili kuwa jumuishi na endelevu na hatimaye kurahisisha shughuli za kiuchumi, kuboresha maisha ya Watanzania na kupunguza umasikini.



Askofu wa Kanisa Katoliki Jimbo la Zanzibar, Augustino Shao akinyunyizia maji ya baraka kwenye hafla ya uwekaji wa jiwe la msingi la kanisa la Mt. Anthony wa Padua, Machui, Zanzibar jana. **PICHA: MARTIN KABEMBA**

# Mfumuko wa bei washuka hadi asilimia 5.10

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MKUU wa Kitengo cha Takwimu za Bei kutoka Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Salma Saleh Ali amesema mfumuko wa bei kwa kipindi cha Februari mwaka huu umeshuka hadi asilimia 5.10 kutoka asilimia 5.26 kipindi cha Januari.

Alitoa takwimu hizo juzi visiwani hapa alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake Mazizini

Salma alisema kushuka kwa kiwango cha mfumuko wa bei kulichangiwa zaidi na kushuka kwa bei za bidhaa za vyakula na vinywaji visivyo na vileo kwa asilimia 8.66 kwa kipindi cha Februari 2024, ikilinganishwa na asilimia 8.98 kipindi cha Januari.

Alisema, faharisi za bei zimeongezeka kufikia 109.53 kipindi cha Februari 2024 ukilinganisha 104.22 kipindi kama hicho mwaka jana.

Alisema mfumko wa bei wa bidhaa za chakula wa mwaka ulioshia Februari 2024 umepungua na kufikia asilimia 8.88 ikilinganishwa na asilimia 9.21 iliyorikodiwa kipindi cha Januari 2024.

Alisema faharisi za bei za chakula kwa kipindi cha Februari 2024 ziliongezeka na kufikia 116.83 kutoka 107.30 katika kipindi cha Januari 2023.

Aidha, alisema mfumuko wa bei wa bidhaa zisizo za chakula kwa mwaka umepungua na kufikia asilimia 2.40 kwa kipindi cha Februari 2024 ikilinganishwa na asilimia 2.46 katika kipindi cha Januari 2024.

"Faharisi za bei za bidhaa zisizo za chakula zimeongezeka na kufikia 104.56 kwa kipindi cha Februari 2024 ikilinganishwa na asilimia 102.11 katika kipindi cha Februari 2023" alisema.

Alizitaja bidhaa zilizosababisha kupungua kwa mfumko wa bei ni mchele (11.0%), unga wa ngano (4.2%), unga wa sembe (5.5%), ndizi za mtwike (25.5%), na mafuta ya kula (6.7%).

Naye Meneja Msaidizi, Uchumi kutoka Benki Kuu ya Tanzania (BoT) Zanzibar, Shami Chamicha, alisema kupungua kwa kasi ya mfumko wa bei ni hatua nzuri ya kiuchumi na malengo yaliokuwepo ya kubakia kwenye tarakimu moja.

"Ni ahueni kwa wananchi na hii inatokana na kuwepo kwa bidhaa za kutosha kwenye masoko. Lakini kwa ujumla hali ya uchumi imeendelea kubakia vizuri na hata upatikanaji wa dola hivi sasa upo vizuri" alisema.

Mchumi Mkufunzi Mwandamizi kutoka Shule ya Biashara, Dk. Estella Ngoma Hassan, alisema kushuka huko kwa kiwango cha mfumko ni hali ya kawaida kulingana na mwenendo wa kibiashara.

Aidha, alisema kuwepo kwenye tarakimu moja ni njia bora ya kuwavutia wawekezaji kwa ajili ya kuwekeza nchini kwa ajili ya maendeleo ya taifa.

Alisema mfumko wa bei wa Zanzibar ni kipimo kinachopima mabadiliko ya bei za bidhaa na huduma mbalimbali zinazokusanywa katika masoko ya Zanzibar.

# M/kiti ACT-Wazalendo ataka kuibuliwa matatizo katika jamii

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

MWENYEKITI wa Chama cha ACT-Wazalendo, Othman Masoud Othman, amewataka viongozi wa chama hicho kujitahidi kuwa sauti ya wananchi kwa kuibua matatizo yanayowakabili na kuyawasilisha ili serikali kuchukua hatua.

Othman ambaye pia ni Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar aliyasema hayo jana huko Shakani Wilaya ya Magharib B Unguja alipofanya majumuisho ya ziara yake ya kuwatembelea wagonjwa, wajane watu wanaoishi katika mazingira magumu, ikiwa ni utaratibu wa chama hicho uliowekwa na mtangulizi wake Hayati Maalim Seif Sharif Hamad.

Othman alisema katika ziara hiyo ameshuhudia changamoto kadhaa kutoka kwa wananchi ambazo zimemfunza kwamba yanahitaji kusimamiwa na viongozi katika ngazi mbalimbali hasa kutokana na kwamba wapo wananchi wengi ambao wanaishi katika maisha duni.

Alisema ni wajibu wa viongozi kushirikiana ili matatizo ya wananchi walionayo wanajitahidi kuandaa mikakati na mipango iliyosahihi na madhubuti na kufanya kazi ya kuwa sauti ya wananchi katika kuzifikia na kuzitatua changamoto za wananchi zinazowakabili katika maeneo yao wanayoishi.

Alisema pia amejifunza na kushuhudia shida na changamoto za wananchi zilizopo katika maisha yao ya kila siku ambazo nyingine siyo kwamba zimeshindikana kutatuliwa, lakini inatokana na baadhi ya watendaji kutokujali na kufanya kazi zao kwa kuwajibika kwa umakini katika kuzikabili shida hizo.

Othman aliwataja watendaji hao kuwa ni katika ngazi mbali mbali za serikali za mitaa, shehia na serikali kuu ambapo ingewezekana kuchukuliwa hatua kwa matatizo ambayo wananchi wanakabiliana nayo na kutatutuliwa.

Aidha, Othman alisema hivi sasa Zanzibar wananchi wanaendelea kukumbwa na tatizo kubwa la maradhi yasioyoambukiza ikiwemo changamoto ya kisukari, mgongo, mifupa pamoja na kupooza akisema kwamba ni maradhi yanahitaji kinga zaidi kuliko tiba.

Alisema kwamba maradhi hayo yanahitaji kinga zaidi lakini pia yanapotokea bado matibabu yake ni changamoto zaidi kwa wananchi hasa katika utumiaji wa dawa kwa kuzingatia utaratibu sahihi kama inavyoelekezwa na wataalamu.

Mwenyekiti wa ACT-Wazalendo Mkoa wa Magharib B kichama, Ali Juma, alisema Zanzibar inaendelea kuwa na umasikini ambao unaweza kuondolewa kwa kuwepo juhudi za pamoja na za Wazanzibar.

Aidha alimpongeza mwenyekiti huyo kutokana kufanya ziara hiyo katika mikoa yote kichama na kutekeleza majukumu yake mbalimbali kwa ufanisi kulingana na malengo ya chama hicho


# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**ASAJILE PIUS MAHENGE** anatangaza kupotelewa kwa hati yake ya kusafiria (PASSPORT) yenye namba **TAE490458** iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Makao Makuu mnamo tarehe 06/07/2022. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/ILA/29691/2024.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**SAMSON ESTOMIH NAFTAL** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S1840/0274** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **KIMASEKI SEKONDARI mwaka 2020.** Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/ARU/ARU/6360/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MOHAMEDI HASSANI MTOPA**

ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA YA USAJILI **T 278 BTA** AINA YA MARK II GRAND RANGI YA FEDHA. CHASISI NAMBA **GX1106059464.** YEYOTE ATAEFANIKIWA KUIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHOPO KARIBU NAE POLISI TAARIFA

**PHQ/IRI/IRI/262292/2023.**

## KADI ZA BAJAJI ZIMEPOTEA

**PIGILIANO VITUS NGILIULE**

anatangaza kupotelewa na kadi za **Bajaji** zenye namba za usajili **MC 314 DDU, MC 701 DDT** aina ya **TVS KING.** Yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo cha polisi.

TAARIFA YA POLISI NI

**PHQ/RUK/SUM/1037/2024.**

## TANGAZO LA KUPOTELEWA NA NYARAKA YA UMILIKI WA KIWANJA

**Nalija Mlapa Ng'osha**

Anatangaza kupotelewa na Nyaraka ya Umiliki wa Kiwanja namba **47 Kitalu "I"** Kilichopo Majengo Manispaa ya Shinyanga. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa Kituo cha Polisi kilichopo karibu au awasiliane na Nalija kwa simu namba **0767-216464.**

Taarifa ya Polisi RB:

**PHQ/SHI/SHI/941/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**EZEKIEL PAUL SIRA**

ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI YENYE NAMBA YA USAJILI **MC940 DBL.** CHASISI NAMBA **LC6PCK766M0003126.** YEYOTE ATAEFANIKIWA KUIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHOPO KARIBU NAE POLISI TAARIFA

**PHQ/IRI/IRI/3673/2024.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO BOMA**

**WILAYA YA MOROGORO**
**MKOA WA MOROGORO**

**Usimamizi wa Mirathi Na...12/2024**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU: JUMA RUZEBELE wa KARUME**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA HAMIS MBARUK**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5 (2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo Tarehe 09 Mwezi 04 Mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Zingatia;

- Endapo kuna yoyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia

Imetolewa leo tarehe 19 mwezi 03 mwaka 2024

---

**FOMU MIRATHI - 2**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika mahakama ya Mwanzo ya wilaya ya TEMEKE**

**Kituo cha JUMUISHI Mkoa DAR ES SALAAM**

**Usimamizi wa Mirathi Na. 367/2024**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU DUSUKI MWINYIGOGO MZEE WA....**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA SALMA KITWANA KALIMA**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 16 mwezi 04 mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Zingatia;

Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta mahakamani kukaguliwa.

Imetokewa leo tarehe 13 mwezi 03 mwaka 2024.

HAKIMU

---

**IN THE DISTRICT COURT OFDODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 6070/2024**

**In the matter of the Estate of the late ELIANAMI DARLINGTON RUSHATSI of Medeli Kisasa within Dodoma Region**

**AND**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY CAROLINE WILFRED TARIMO**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 Probate Rules Gn 369 of 163)**

..........................................................

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 22 ND Day of APRIL, 2024

Date at Dodoma this **20TH Day of MARCH, 2024.**

RESIDENT MAGISTRATE

---

**IN THE DISTRICT COURT OF KYELA**
**AT KYELA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 5692 OF 2024**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE NEEMA JOLESI SANGA**

**AND**

**In the matter of Application for Letters of Administration by DEBORA NIKORAUS MAHENGE........PETITIONER**

**GENERAL CITATION (RULE 75)**

All persons claiming to have any interest in the estate of above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of Administration) is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 29th of April, 2024.

Dated at Kyela this 25th day of March, 2024.

SENIOR RESIDENT MAGISTRATE
KYELA.

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**EFER TRADERS CO. LTD**

inatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili

**T 733 EDG – TOYOTA HARRIER.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote che polisi. Taarifa ya polisi:

**PHQ/DAR/KIN/48701/2024.**

---

**IN THE DISTRICT COURT OF KYELA**
**AT KYELA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 5693 OF 2024**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE FORDIA JOHN MWAKASENDILE**

**AND**

**In the matter of Application for Letters of Administration by ALESI MWESIMPYA........PETITIONER**

**GENERAL CITATION (RULE 75)**

All persons claiming to have any interest in the estate of above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of Administration) is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the **29th of April, 2024.**

Dated at Kyela this **25th day of March, 2024.**

SENIOR RESIDENT MAGISTRATE
KYELA.

***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie, 0782253676***

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.

TUPIGIE: +255 - 0677 020701

AU

TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO, MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**
**website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

Kwa

## Waziri kuongoza usambazaji mitungi ya gesi kwa wananchi

**Na Mary Geofrey**

NAIBU Waziri wa Nishati, Judith Kapinga ameahidi kuongoza kwa ufanisi usambazaji mitungi ya gesi takribani 10,000 iliyotolewa na kampuni ya Taifa Gas hivi karibuni kwa ajili ya wananchi katika maeneo mbalimbali nchini.

Mitungi hiyo iliyopokewa hivi karibuni na Makamu wa Rais, Dk. Phillip Mpango, kampuni hiyo ikilenga kuunga mkono kampeni ya kumtua kuni mama kichwani inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan.

Kampeni hiyo inalenga kusaidia na kuwezesha wananchi kufikia nishati safi kwa urahisi.

Kapinga alitoa ahadi hiyo katika kikao chake na maofisa waandamizi wa kampuni ya Taifa Gas, wakiongozwa na Meneja Mkuu wa kampuni hiyo, Devis Deogratius walipomtembelea ofisini kwake jijini Dar es Salaam jana.

Mbali na kupongeza kampuni hiyo kwa juhudi zake za kuunga mkono kampeni ya kumtua mama kuni kichwani, Naibu Waziri Kapinga alisema ufanisi wa kampeni hiyo unategemea zaidi ushiriki wa wadau wengi zaidi kwa kuzingatia ukweli kwamba kampeni hiyo inalenga kufikia walengwa kote nchini.

"Kama wizara, tumedhamiria kuhakikisha tunafikia walengwa wote wanaostahili kufikiwa na kampeni hii kama ambavyo Rais Samia alivyokusudia.

"Kwetu imekuwa faraja kubwa kuona wadau kama Taifa Gas wapo nasi bega kwa bega kuhakikisha hilo linafanikiwa. Pamoja na kusambaza mitungi hii ya gesi, pia tutahakikisha elimu kuhusu nishati safi ya kupikia inafikia walengwa kila wilaya na kila kata," alisema.

Kapinga alitoa wito kwa kampuni ya Taifa Gas kuhakikisha inaongeza zaidi vituo vya kujazia gesi katika maeneo mbalimbali nchini, ili wananchi wengi zaidi wafikiwe na huduma ya nishati hiyo kwa urahisi.

Meneja Mkuu wa kampuni hiyo, Devis Deogratius alisema kuwa Taifa Gas itaendelea kushirikiana na serikali katika kuimarisha kampeni ya matumizi ya nishati safi, huku akibainisha kampuni hiyo itaendelea na mkakati wake wa kupanua zaidi uwekezaji wake kwenye maghala yake nchini, ili kuihakikishia nchi usalama na upatikanaji nishati hiyo.

"Tunaelewa kuwa mabadiliko kuhusu matumizi ya nishati yanaendelea kuonekana na yatakuwa taratibu. Cha msingi ni kuweka mikakati ya kuongeza idadi ya watumiaji nishati safi nchini kutoka asilimia nane ya sasa," alisema.



Naibu Waziri wa Nishati, Judith Kapinga (kulia) akipokea nyaraka mbalimbali kuhusu mkakati wa kampuni ya Taifa Gas kufanikisha upatikanaji nishati safi ya kupikia kutoka kwa Meneja Mkuu wa kampuni hiyo, Devis Deogratius wakati maofisa wa kampuni hiyo walipomtembelea ofisini kwake jijini Dar es Salaam jana. **MPIGAPICHA WETU**

# Mashambulizi yatikisa ukanda wa Gaza usiku

**GAZA,** Palestina

MASHAMBULIZI makali yaliyoambatana na mabomu yanayorushwa kutoka angani na ardhini yameendelea Ukanda wa Gaza katika usiku wa kuamkia jana.

Wakati vikosi vya Israel vinaendelea kuiangamiza Gaza, Marekani na serikali ya nchi hiyo wamekubaliana kupanga upya mazungumzo ambayo yalifutwa kuhusu Opresheni ya kijeshi katika mji wa kusini wa Gaza, Rafah.

Hata hivyo, Marekani imeongeza ukosoaji dhidi ya Waziri Mkuu wa Israel Benjamin Netanyahu, kuhusiana na ongezeko la idadi ya vifo vya raia wa Palestima katika eneo hilo.

Serikali ya Marekani inaonyesha kutounga mkono kutokana na raia wengi kuwa hatarini kukabiliwa na baa la njaa na mipango ya Israel kuendeleza operesheni yake ya kijeshi katika mji wa Rafah, ambao umehifadhi mamilioni ya watu waliokimbia vita.

Mashambulizi hayo yanafanyika licha ya Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa kupitisha azimio linalotaka usitishwaji wa mapigano na kuachiwa kwa mateka wanaoshikiliwa na wanamgambo wa Hamas.

**Mapema jana, jeshi la Israel lilisema wanamgambo wamekuwa wakiwafyatulia wanajeshi risasi kutoka ndani na nje ya wodi ya wagonjwa wa dharura katika hospitali ya Al-Shifa iliyoko mjini Gaza.**

Msemaji wa Ikulu ya Marekani ya White House, Karine Jean-Pierre, alisema serikali ya Netanyahu imerudi nyuma na kukubaliana kupanga upya mkutano wa kujadili operesheni ndani ya Rafah.

Alisema wanashauriana kupanga tarehe ya mkutano huo kufanyika.

"Unaponiuliza kuhusu mikutano ambayo ilifanyika hapa, yalikuwa majadiliano mazuri na waziri wa ulinzi wa Israel katika siku mbili zilizopita. Kwa hiyo sasa tunafanya kazi nao kutafuta tarehe mwafaka ambayo bila shaka itazifaa pande zote mbili. Lakini ofisi ya waziri mkuu imekubali kupanga upya mkutano huo ambao utajadili Rafah, ni jambo zuri." alisema

Msemaji wa Wizara ya Mambo ya Nje ya Marekani, Mathew Miller, alisema wanapanga kuipa Israel mbadala wa operesheni ya Rafah, unaolenga kuyapiga maeneo ya Hamas na wakati huo huo kupunguza vifo vya raia.

Wizara ya afya inayoendeshwa na Hamas ilitoa takwimu yake ikionyesha watu 66 waliuawa usiku wa kuamkia jana.

Mapigano hayo yaliendelea karibu na hospitali tatu za Gaza, na kuongeza hofu kwa wagonjwa, wahudumu wa afya na watu waliochukua hifadhi ndani ya taasisi hizo. Hospitali ya Al-Amal mjini Khan Yunis imesitisha kutoa huduma baada ya raia kuondolewa.

Mapema jana, jeshi la Israel lilisema wanamgambo wamekuwa wakiwafyatulia wanajeshi risasi kutoka ndani na nje ya wodi ya wagonjwa wa dharura katika hospitali ya Al-Shifa iliyoko mjini Gaza.

Aidha, vifaru vya Israel na magari ya kijeshi pia yamekusanyika karibu na hospitali ya Nasser.

Wakati huo huo, mataifa kadhaa yameanza kudondosha msaada, huku njia ya baharini kutoka nchini Cyprus ikitumika kupeleka shehena ya kwanza ya chakula.

Waziri wa Ulinzi wa Marekani, Lloyd Austin, alitoa tahadhari kutokana na idadi ya watu wanaofariki wakati alipokutana na Waziri wa Ulinzi wa Israel, Yoav Gallant.

Hata hivyo, machafuko yameongezeka katika Ukingo wa Magharibi unaokaliwa na Israel, ambako wahudumu wa afya na jeshi walisema watu watatu wamejeruhiwa katika shambulizi la bunduki lililolenga basi jana.

Pia, vita hivyo vimeongeza hofu ya mzozo huo kutanuka na kuwa wa kikanda, hasa katika mpka wa Israel na Lebanon.

Kundi la Hezbollah lenye makazi yake nchini Lebanon limetangaza vifo vya wanachama wake wanane baada ya mapigano yaliyotokea eneo la mpakani kwa muda wa siku moja. **DW**

# MASHABIKI LIGI KUU WAITWA KUZISHANGILIA SIMBA, YANGA

**Na Shufaa Lyimo**

MASHABIKI wa soka na wadau mbalimbali wa michezo nchini wametakiwa kujitokeza kwa wingi kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa leo ili kuishangilia Simba itakayowavaa Al Ahly katika mechi ya hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Wito huo pia umetolewa kwa mashabiki hao kufika kwa wingi kesho wakati Yanga itakapowakaribisha Mamelodi Sundowns kutoka Afrika Kusini katika mechi ya hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Akizungumza na Nipashe jana, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Ligi Kuu Tanzania (TPBL), Almasi Kasongo, alisema jana kwa umoja wa mashabiki anaamini utasaidia timu hiyo kuingia hatua ya nusu fainali katika michuano hiyo.

**"Ninasisitiza Watanzania wajitokeze kwa wingi kesho (leo), kwa ajili ya kuishangilia timu yetu (Simba), kwa sababu kushinda kwake ni furaha kwa taifa letu kiujumla," alisema Kasongo.**

Aliongeza viongozi wa soka wamejipanga kuhakikisha wanawachukulia hatua mashabiki ambao watakosa uzalendo wa wawakilishi hawa na nchi.

"Tunawaomba mashabiki wafike kwa wingi uwanjani kuishangilia Simba, na keshokutwa (kesho), kuishangilia Yanga, lakini hatutawafumbia macho kwa wale watakaokwenda kinyume na matakwa ya nchi kwa kuishangilia Al Ahly badala ya Simba," Kasongo alisema.

Aliongeza Simba ina uwezekano mkubwa wa kusonga mbele kwa sababu itacheza mechi hiyo kwenye uwanja wake wa nyumbani.

Alisema maandalizi na hamasa mbalimbali yaliyofanywa na viongozi wa Simba yatasaidia kuwapa nguvu wachezaji ili kufanya vyema watakapokuwa uwanjani kuwakabili Waarabu hao kutoka Misri.

"Ninapenda kuwakumbusha wachezaji kufuata vyema maelekezo waliyopewa na benchi lao la ufundi, ninawaomba wacheze kwa kujiamini ili wafanikishe malengo yao, kama nchi tuko pamoja katika michuano hii," Kasongo alisema.

Hii ni mara ya kwanza kwa timu mbili za Ligi Kuu Tanzania Bara kucheza robo fainali ya michuano hiyo ya kimataifa inayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).



Wachezaji wa mpira wa miguu vijana kutoka sehemu mbalimbali jijini, Dar es Salaam wakifanya mazoezi kwenye Uwanja wa Karume ili kuimarisha vipaji vyao. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Mashujaa yaipigia hesabu Coastal Union*

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kumaliza mapumziko ya muda mfupi, kikosi cha Mashujaa kimeanza rasmi mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara pamoja na michuano ya Kombe la FA, imeelezwa.

Mashujaa itaivaa Coastal Union katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa Aprili 12, mwaka huu kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika mkoani, Kigoma.

Kocha Mkuu wa timu hiyo, Abdallah Mohamed 'Bares,' alisema jana kikosi hicho kimerejea mazoezini na kimeanza kufanya programu maalumu ya ufukweni.

Bares alisema kitu cha kwanza anachokiangalia ni utimamu wa mwili kwa sababu wachezaji wake wamekaa muda mrefu bila kupata mechi, hivyo kabla ya kuwapeleka uwanjani ni lazima wawe fiti.

"Tumerejea, lakini tuko Dar es Salaam, tumeanza mazoezi kwenye ufukwe wa Coco ili kupata utimamu wa mwili na baada ya hapo tutarejea uwanjani, nadhani tutapata pia mechi za kirafiki kabla ya kurejea Kigoma," alisema Bares.

Mashujaa imebakisha mechi tisa ili kumaliza msimu huu, ipo nafasi ya 12 katika msimamo wa Ligi Kuu Bara, ikiwa moja ya timu ambazo zipo kwenye hatari ya kushuka daraja au kwenda kucheza michezo ya mchujo.

Maafande hao watamalizia msimu nyumbani Mei 29, mwaka huu kwa kuikaribisha Dodoma Jiji.

## CHANEZA yawaita wadau kugombea

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

CHAMA cha Netiboli Zanzibar (CHANEZA), kinawaomba wadau wa mchezo huo kujitokeza kuwania nafasi mbalimbali za uongozi katika chaguzi za kuanzia ngazi ya wilaya ambazo zitafanyika hivi karibuni.

Katibu Mkuu wa CHANEZA, Said Mansab, tayari zimeshafanyika chaguzi katika wilaya nne za Kisiwa cha Pemba na kuitaja Wilaya ya Mkoani ndio iliyobakia kukamilisha mchakato huo.

Mansab alisema wamebaini katika chaguzi zilizofanyika kumekuwa na mwamko mdogo wa wagombea na sasa wanawaomba wadau kujitokeza ili kupata viongozi watakaosimamia vizuri mchezo huo.

"Lazima tuje na mpango utakaosaidia wadau wa mchezo huu kugombea nafasi mbalimbali za uongozi, tulijua tutakutana na changamoto hii ya wajumbe wachache kujitokeza kwa sababu hii ni mara ya kwanza kwa wilaya kufanya chaguzi," alisema kiongozi huyo.

Aliongeza utaratibu huu umeanza mwaka huu kutokana na mabadiliko ya katiba ya CHANEZA kama ilivyoelekezwa na Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Michezo Zanzibar.

## Ligi ya Wushu 2024 kufanyika Mei Mosi Dar

**Na Shufaa Lyimo**

WAKATI Ligi ya Wababe wa Kitaa (WWK) ya mchezo wa wushu imepangwa kufanyika ifikapo Mei Mosi, mwaka huu jijini, Dar es Salaam, mshindi wa kwanza atapata zawadi ya Sh. milioni 2.5, imeelezwa.

Mshindi wa pili ataondoka na zawadi ya Sh. milioni 1.5 na mchezaji atakayemaliza katika nafasi ya tatu atajinyakulia Sh. milioni moja.

Akizungumza jijini, Dar es Salaam jana, Katibu Mkuu wa Chama cha Wushu Tanzania (TWA), Sempai Kapipi, alisema ligi hiyo itashirikisha wapiganaji kutoka katika mitaa mbalimbali ya Tanzania Bara.

Kapipi alisema uzito utakaopiganiwa ni kuanzia kilo 52 hadi 60 na kila kundi litashirikishia wachezaji 16 huku ligi hiyo ikitarajiwa kuchezwa kila baada ya miezi mitatu.

Aliitaja baadhi ya michezo itakayochezwa siku hiyo ni pamoja na Karate, Kungfu, Kick Boxing, Taekwondo, Jujitsu na Muay Thai Sand.

Naye Mwenyekiti wa TWA, Mwarami Mitete, alisema ujio wa ligi hiyo utaleta chachu kwa vijana kwa sababu watu wenye sanaa za mapigano wataonyesha vipaji vyao.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### ARSENAL KUSAJILI WAPYA 10

ARSEAL ina orodha ya wachezaji 10 wanaowania nafasi ya mshambuliaji mpya msimu huu wa joto huku Mslovenia wa RB Leipzig, Benjamin Sesko, 20, Viktor Gyokeres wa Sporting Lisbon (25) na mwenzake wa Sweden, Alexander Isak (24) wa Newcastle wakiwa miongoni wanaofuatiliwa. ***(Mirror)***

### YAMTAKA BRANTHWAITE

KLABU ya Manchester United inamtaka beki wa kati wa Everton, Jarrad Branthwaite, 21, huku wakiweka kipaumbele katika kuboresha safu yao ya ulinzi kwa ajili ya msimu ujao. ***(Telegraph)***

### AMVUTIA GUARDIOLA

PEP Guardiola anavutiwa na kiungo wa Newcastle United, Bruno Guimaraes, 26, lakini Manchester City italazimika kulipa euro milioni 100 ili kumsajili mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil. ***(Fichajes)***

### PAQUETA ANUKIA CITY

KLABU ya West Ham inatarajia Manchester City kutaka tena huduma za kiungo wao wa kati wa Timu ya Taifa ya Brazil, Lucas Paqueta, 26. ***(Football Insider)***

### DIAZ AITAMANI LALIGA

MSHAMBULIAJI wa Liverpool, Luis Diaz, 27, hajakata tamaa ya kuhamia moja ya katika timu kubwa nchini Hispania kwa siku zijazo, kwa mujibu wa baba yake mchezaji huyo wa kimataifa wa Colombia. ***(Daily Mail)***

### BENTO ATAKIWA CHELSEA

CHELSEA ni moja ya timu zinazomhitaji golikipa wa Athletico Paranaense, Bento, 24, ambaye alicheza mechi yake ya kwanza Brazil dhidi ya England wiki iliyopita. ***(Globo)***

### GIMENEZ KUMRITHI KANE

KLABU ya Tottenham Hotspur inataka kumsajili mshambuliaji wa Feyenoord raia wa Mexico, Santiago Gimenez, 22, kama mbadala wao wa Harry Kane katika msimu huu wa joto, ikiwa ni mwaka mmoja baada ya mshambuliaji huyo wa England kujiunga na Bayern Munich. ***(Caught Offside)***

### ANSELMINO ANUKIA UNITED

MANCHESTER United imeonyesha nia ya kumsajili beki wa Timu ya Taifa ya Argentina, Aaron Anselmino, mwenye umri wa miaka 18 ambaye kwa sasa anaitumikia Boca Juniors. ***(Ole)***

### JORGINHO KUREJEA BRAZIL

KIUNGO wa kati wa Timu ya Taifa ya Italia, Jorginho, 32, anaweza kuondoka Arsenal msimu huu na kurejea katika nchi yake.***(Football London)***

### ILING-JUNIOR AGEUKA LULU

TOTTENAHAM Hotspur, West Ham, Brighton na Everton zote zinapanga kumsajili winga wa Juventus na Timu ya Taifa ya England, Samuel Iling-Junior, 20. ***(Football Insider)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# DE BRUYNE FITI KUIVAA ARSENAL

## Kurejea kwa nyota huyo kutaipunguzia City presha ya mchezo...

**MANCHESTER,** England

MANCHESTER City ina matumaini nyota wake, Kevin De Bruyne, atakuwa fiti kwa ajili ya mechi muhimu ya Ligi Kuu England dhidi ya Arsenal itakayochezwa keshokutwa, kwa mujibu wa ESPN.

**De Bruyne alikosa katika ushindi wa robo fainali ya michuano ya Kombe la FA dhidi ya Newcastle United kwa sababu ya jeraha la nyonga, huku tatizo hilo pia likimkosesha nafasi ya kucheza mechi za kirafiki kati ya Ubelgiji dhidi ya Jamhuri ya Ireland na England wakati wa mapumziko ya kimataifa.**

Lakini kuna matumaini yanayoongezeka kuhusu kiungo huyo huenda atapatikana kwa ajili ya mchezo huo baada ya kufanya mazoezi na kikosi cha wachezaji wa umri chini ya miaka 23 mapema wiki hii.

Jack Grealish, ambaye hakuwa sehemu ya kikosi cha England alipokuwa anaendelea kupata nafuu kutokana na jeraha la misuli, pia amekuwa akifanya mazoezi katika akademi ya City wiki hii.

Madaktari wataendelea kumfuatilia De Bruyne, lakini jana alitarajiwa kushiriki mazoezi ya kikosi cha kwanza.

Wachezaji wengi wa kimataifa wa City wanatarajiwa kurejea klabuni hapo leo kabla ya maandalizi yao ya mwisho ya mchezo dhidi ya Arsenal utakaochezwa kwenye dimba la Etihad.

Uwezekano wa uwepo wa De Bruyne ni nyongeza kwa Pep Guardiola, ambaye anatoa jasho kutokana na utimamu wa Kyle Walker na John Stones.

Walker alilazimika kutolewa nje wakati England ilipochapwa 1-0 na Brazil Jumamosi iliyopita baada ya kupata jeraha la misuli ya paja, huku Stones akitolewa mapema wakati wa sare ya 2-2 na Ubelgiji Jumanne iliyopita kutokana na tatizo la kifundo cha mguu.

Jeraha la Walker halifikiriwi kuwa mbaya, lakini bado anakabiliwa na mbio dhidi ya wakati ili kudhibitisha usawa wake kabla ya kukabiliana na wapinzani wao wa taji vijana wa Mikel Arteta.

# GIROUD AKARIBIA KUTUA MAREKANI




**NEW YORK,** Marekani

KLABU ya LAFC ya Ligi Kuu ya Soka Marekani (MLS), inakamilisha makubaliano na AC Milan kuhusu kumsajili mshambuliaji wa kimataifa wa Ufaransa, Olivier Giroud, vyanzo vimeithibitishia ESPN.

Giroud mwenye umri wa miaka 37, anatarajiwa kujiunga na LAFC baada ya kukamilisha majukumu yake katika Timu ya Taifa ya Ufaransa kwenye michuano ya Euro 2024, inayotarajiwa kufanyika kuanzia Juni 14 hadi Julai 14, mwaka huu.

Dirisha la usajili la majira ya joto la MLS linafunguliwa Julai 18 na kufungwa Agosti 14, mwaka huu.

Mkataba atakaosaini Giroud unatarajiwa kudumu angalau hadi mwisho wa msimu wa mwaka 2025.

Mkataba wake wa sasa na AC Milan unamalizika mwishoni mwa msimu wa 2023-24 wa Serie A.

Giroud amekuwa mfungaji mzuri wa mabao kwa Ufaransa na klabu alizozitumikia, akifunga mabao 276 katika maisha ya klabu ambayo amecheza takriban mechi 700 za ligi na mataji, na ndiye mfungaji bora wa muda wote wa Ufaransa akiwa na magoli 57 katika mechi 131.

Alikuwa sehemu ya kikosi cha Ufaransa kilichoshinda Kombe la Dunia mwaka 2018, na ameshinda jumla ya mataji 11 akiwa na klabu tofauti, zikiwamo Montpellier, Arsenal, Chelsea na Milan, ambapo alisaidia kushinda Serie A msimu wa 2021-22.

Giroud pia aliiwakilisha Ufaransa katika michuano mingine miwili ya Kombe la Dunia na michuano mitatu ya Ulaya.

Msimu huu, Giroud amekuwa katika kiwango bora, akifunga mabao 12 na kutoa pasi nane za mabao katika mechi 26 za Serie A.

# Nitastaafu nisipoweza kuisaidia timu - Messi

**MIAMI,** Marekani

LIONEL Messi amesema umri hautachangia katika uamuzi wake wa kustaafu na atajua ni lini wakati sahihi wa 'kutundika daruga' pale atakapoona hana mchango wowote katika mafanikio ya timu yake.

Nahodha huyo wa Argentina mwenye umri wa miaka 36, hajatoa dalili kuhusu ni lini atastaafu, huku mkataba wake na Inter Miami utamalizika ifikapo Desemba mwakani.

"Nitajua basi wakati ninapojua sifanyi maonyesho, sifurahii, siwasaidii wachezaji wenzangu," alisema Messi akiiambia Big Time Podcast ya MBC.

"Ninajikosoa sana, najua ninapokuwa mzuri na mbaya, ninapocheza vizuri, na ninapocheza vibaya... Na nikihisi ni wakati wa kuchukua hatua hiyo, nitaichukua bila kufikiria, lakini sio kuhusu umri.

"Nikijisikia vizuri, nitajaribu daima kuendelea kushindana, kwa sababu hiki ni kile ninachopenda na kile ninachojua kufanya."

Messi ambaye ni mshindi mara nane tuzo ya Ballon d'Or, ambaye alikuwa nahodha wa Argentina na kutwaa ubingwa wa Kombe la Dunia 2022, anatarajiwa kuingoza timu yake ya taifa kwenye michuano ya Copa America msimu huu.

"Kama mambo hayangeenda jinsi tulivyofanya katika dimba la Qatar, ningeiacha timu ya taifa," aliongeza Messi.

Messi yuko nje ya uwanja kutokana na jeraha la misuli ya paja na alikosa mechi mbili za kirafiki za timu yake ya taifa dhidi ya El Salvador na Costa Rica.



# Baba ampeleka Diaz Madrid



**MADRID,** Hispania

BABA mzazi wa Luis Diaz amefungua milango ya kuhamia Hispania kwa fowadi huyo wa Liverpool, akifichua anatumaini mwanawe atacheza LaLiga siku moja.

Diaz alijiunga na Wekundu hao katika dirisha la uhamisho la Januari mwaka, 2022 na kuisaidia klabu hiyo kutwaa Kombe la FA na Kombe la Carabao katika nusu msimu wake wa kwanza alipotua Anfield, pia akianzia kwenye kichapo cha 1-0 katika fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Real Madrid mwaka huo.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Colombia amekuwa akihusishwa na kuondoka Merseyside, huku tetesi zikisema Paris Saint-Germain wanamtaka.

Hata hivyo, baba yake, Luis Manuel, amedokeza mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 huenda akahamia LaLiga.

Alisema: "Wakati anaondoka Porto sikujua kulikuwa na kitu kizuri na klabu ya Madrid. Nilisikia mambo, lakini sikuwahi kujua kama kulikuwa na kitu kingine. Nikiwa na Liverpool kila kitu kilikuwa sahihi zaidi.

"Agizo lilikuwa sahihi zaidi kwa Luis kufika huko. Ilitarajiwa angeweza kuja hapa Hispania. Radamel Falcao alikuwa tayari amekuwapo, James Rodriguez, pia, lakini bado sijakata tamaa."

Baba huyo hapo awali alifichua nyota huyo alikuwa na ndoto ya kuichezea Barcelona, akiwa shabiki wa wababe hao wa Katalunya tangu akiwa mtoto, ingawa pia alishukuru Liverpool na Porto kwa kumwongoza winga huyo katika maisha yake yote ya soka.

Alisema: "Ukweli najua kidogo sana kuhusu Barcelona kwa sasa. Ni kweli Luis ni shabiki mwaminifu wa Barcelona na ingekuwa ndoto yake kwenda huko. Hadi sasa ningependa kuwashukuru Porto na Liverpool kwa jinsi walivyomkaribisha na kumpokea.

Mkataba wa sasa wa Diaz Liverpool bado una zaidi ya miaka mitatu kumalizika, akiwa amefunga mabao 22 katika mechi 86 alizoichezea Wekundu hao.

## Simba, Al Ahly ni zaidi ya vita

INATOKA UKURASA 24

African Football League (AFL), mara mbili na michezo yote kutoka sare. Koller alisema wanatambua ubora wa Simba na kutokana na kipindi cha hivi karibuni kuonyeshana ushindani, kikosi chake kinatakiwa kuongeza umakini kuhakikisha wanafanya vizuri katika mchezo wa leo.

"Nimecheza nao mechi mbili na zote nimetoka nao sare, niliwaona na naweza kusema wapo kwenye 'levo' kama yetu na wala sio timu ndogo. Tunawaheshimu na tutacheza kwa umakini mkubwa. Ni kweli tutakosa wachezaji muhimu lakini hatuna presha juu ya kutokuwepo kwao kwa sababu kuna mbadala wao," alisema kocha huyo.

## Kouassi fiti 100% kuivaa Mamelodi

INATOKA UKURASA 24

Ivory Coast, kwa hiyo hana tatizo lolote. Ila kucheza sasa ni uamuzi wa Kocha Mkuu (Miguel Gamondi), kama atamtumia kwa dakika zote 90 au atamtumia kipindi cha pili, au yeye mwenyewe atakavyoona inafaa," alisema Kamwe.

Ofisa huyo alionyesha kushangaa baadhi ya taarifa kuhusu Bacca hatocheza mechi ya kesho kutokana na kuwa na kadi tatu za njano.

"Bacca atacheza mechi hiyo kwa sababu si kweli kama ana kadi hizo, badala yake ana kadi mbili tu za njano alizozipata katika mechi ya hatua ya makundi dhidi ya Al Ahly na CR Belouizdad.

Jumla ni ana kadi tano za njano, alipata tatu mwanzo na akaukosa mchezo dhidi ya Medeama, ikaua zile za mwanzo, baada ya hapo ndipo akapata dhidi ya Wamisri na Waalgeria, ufafanuzi ndio huo, lakini kwa kuongeza tu kanuni ya msimu huu ya ligi hiyo wanafuta kadi zote za makundi kama hazimsimamishi mchezaji kucheza mechi inayofuata hatua ya robo fainali na kwa sababu alikuwa na mbili, ina maana hata zile mbili alizonazo zimeshafutwa," alifafanua Kamwe.

Kuelekea mchezo huo, Kamwe alisema maandalizi yamekuwa 'makubwa' na mara ya mwisho aliona aina hiyo ya maandalizi walipocheza mechi ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya TP Mazembe.

"Kocha wetu Gamondi ametuambia, hatuwezi kuwaangusha Watanzania katika ardhi ya nyumbani. Na mimi nimeongea na wachezaji wanasema wanakwenda kucheza mchezo kama hakuna tena mechi nyingine mbele yao, dhamira yao ni moja tu, kupata matokeo katika mechi ya kwanza," Kamwe alisema.

Aliongeza wapinzani wao Mamelodi Sundowns wameshawasili nchini tayari kwa ajili ya mchezo huo wa kimataifa.

# OKWI AWAAMBIA SIMBA HUU NI MWAKA WAO CAF

**Na Saada Akida**

MSHAMBULIAJI wa zamani wa Simba, Emmanuel Okwi, ambaye kwa sasa anaichezea Erbil SC ya Iran, amesema Wekundu wa Msimbazi wana nafasi kubwa ya kuibuka na ushindi katika mechi yao ya hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Al Ahly kutoka Misri itakayochezwa leo kwenye dimba la Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Nyota huyo aliyeitumikia Simba kwa misimu mitatu tofauti ikiwamo aliliambia Nipashe jana Al Ahly ni timu kubwa na imekuja Tanzania mara nyingi katika miaka ya karibuni hivyo wenyeji wanajua namna ya kuwakabili.

**Hata hivyo, Okwi alisema baada ya Al Ahly kushindwa kuondoka na ushindi kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa katika mechi zake za hivi karibuni, Simba wanatakiwa kucheza kwa tahadhari kwa sababu anaamini safari hii Waarabu hao watakuja kwa nguvu zaidi ili wafanikiwe kusonga mbele na kwenda kutetea ubingwa wao.**

Okwi alisema Simba ina rekodi nzuri inapocheza kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, imezifunga timu nyingi lakini wachezaji wanapaswa kutambua umuhimu wa mchezo ulioko mbele yao, awataka wajitume na kufuata vyema maelekezo ya mwalimu .

"Wachezaji wanapaswa kuingia kwa tahadhari kwa sababu wanaenda kukutana na bingwa mtetezi wa mashindano, hivyo haitakuwa rahisi, uzuri wanaenda kupata faida ya mashabiki mara nyingi wamekuwa wakijitoa sana," alisema Okwi.

Aliongeza Simba ina wachezaji wakubwa na wenye uzoefu wa mashindano hayo na sasa wanapaswa kutumia kila nafasi watakazopata lakini pia wasifanye makosa katika eneo la ulinzi.

"Katika mpira kila kitu kinawezekana, kama watu wakiweka nia na sisi tutakuwa pamoja nao kwa kuwaombea ili wafanye vizuri na kutinga nusu fainali kwa mara ya kwanza," alisema mshambuliaji huyo wa ambaye pia aliwahi kuitumikia Yanga.

Akiwa Simba, Okwi, ambaye ni raia wa Uganda alifunga mabao muhimu na kuwafanya mashabiki na wanachama wa timu hiyo wampende katika kipindi chote alichoitumikia timu yao.




Msemaji wa Yanga, Ali Kamwe akiwa amembeba shabiki wa timu hiyo, Suda Hassan, alipokuwa kwenye matembezi ya kuhamasisha mashabiki kujitokeza uwanjani watakapokutana na Mamelodi Sundowns katika mechi ya hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika itakayochezwa kesho. **PICHA: MTANDAO**

## *Tabora Utd mipango itatimia*

**Na Saada Akida**

KOCHA mpya wa Tabora United, Denis Laurence, ameanza kuipigia hesabu michezo tisa ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyobakia pamoja na mashindano ya Kombe la FA, kwa kuahidi kikosi chake kitafanya vizuri.

Katika michuano ya Kombe la FA, Tabora United itakutana na Singida Fountain Gate.

Akizungumza na gazeti hili jana, Laurence alisema katika muda wa siku saba aliokaa na timu hiyo, ameridhishwa na viwango vya wachezaji wake kutokana na kujituma kwenye mazoezi wanayofanya.

Laurence alisema ameshangazwa kuona kwa kipindi kifupi wachezaji wake wamemwonyesha ushirikiano mzuri na pia wanafuata vyema maelekezo anayowapa lakini hajapata changamoto yoyote hadi sasa.

"Ushirikiano ambao wachezaji wananipa unatoa taswira njema kuelekea katika mechi zilizoko mbele yetu, nafurahi kuona wachezaji wananisikiliza vizuri, tunakwenda sawa, tunazungumza lugha moja, hii kwangu ni kubwa sana kama kocha, muhimu nazidi kuwasisitiza kila mmoja ana nafasi katika kikosi changu cha kwanza," alisema Laurence.

Tabora United itakuwa ugenini kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini, Mwanza Aprili 4, mwaka huu kucheza dhidi ya Singida Fountain Gate na itashuka dimbani tena Aprili 14, mwaka huu kuwavaa JKT Tanzania katika mechi ya Ligi Kuu Bara.

Michezo
Ijumaa Machi 29, 2024
Nipashe



De Bruyne fiti kuivaa Arsenal UKURASA 21



Koller



Benchikha

## Kouassi fiti 100% kuivaa Mamelodi

**Na Adam Fungamwango**

IKIWA imebakia siku moja tu kabla ya kuivaa Mamelodi Sundowns kutoka Afrika Kusini katika mechi ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Yanga imetangaza hali ya beki wake, Yao Kouassi, imeimarika na sasa yupo fiti kwa ajili ya mchezo huo.

Mbali na hilo, klabu hiyo pia imeweka wazi sintofahamu ya beki wake kisiki, Ibrahim Hamad 'Bacca' kuhusu nafasi yake ya kucheza kutokana na kadi tatu za njano alizoonyeshwa.

Pacome na Yao, waliwapa wasiwasi na hofu wanachama na mashabiki wa Yanga, baada ya kuumia katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Azam FC iliyochezwa Machi 17, mwaka huu.

Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe, alisema jana Yao amepona na wasiwasi waliokuwa nao umemalizika kama ilivyokuwa na nyota, Pacome Zouzoua.

"Habari njema kwa wanachama na mashabiki wa Yanga, ni hali ya Yao, yupo fiti kabisa na mimi ndio niliyekwenda kwenye Uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere kumpokea mwenzake, Pacome anayerejea kutoka kwenye kikosi cha Timu ya Taifa ya

INAENDELEA UKURASA 23

# Simba, Al Ahly ni zaidi ya vita

## Makocha wafunguka ni mechi ngumu, rekodi ya African Football League yatajwa...

**Na Saada Akida**

NI siku nyingine iliyokuwa inasubiriwa na mashabiki wa soka nchini kushuhudia Simba ikisaka historia kwa kuivaa Al Ahly kutoka Misri katika mechi ya robo fainali mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika itakayochezwa leo kuanzia saa 3:00 usiku kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

**Dhamira na malengo ya Simba ni kupata ushindi mnono katika dimba la nyumbani kabla kwenda kumalizika dakika 90 za marudiano ugenini Misri.**

Katika siku za hivi karibuni, timu hizo zimekutana mara sita na kila mmoja ameshinda mechi mbili na kutoka sare mbili, jumla mabao ya kufunga yakiwa 14, Simba akifunga matano na Al Ahly ikitikisa nyavu za Wekundu wa Msimbazi mara tisa.

Kila mmoja ana historia ya kutumia vizuri uwanja wake wa nyumbani, Simba inaingia katika kumbukumbu za Tangu Mwaka 1993 ilipofuzu hatua ya Robo fainali kwa kumtoa mpinzani wa muda mrefu wa Al Ahly, Zamalek ya Misri.

Simba imeendelea kuwashangaza wageni kwa rekodi nzuri wanapokuwa nyumbani hasa katika michuano ya kimataifa hadi kuonekana wanapokuwa Dar es Salaam ni sawa na wako 'machinjioni' na kuzaa kauli mbiu maarufu ya 'Kwa Mkapa Hatoki Mtu.'

Al Ahly wao si wageni wa mashindano haya na mara nyingi huonekana wanakuwa 'moto' zaidi wanapofika hatua hii ya mtoano, wakiwa na rekodi ya kutwaa makombe mengi zaidi kuliko timu nyingine Afrika, wakibeba ubingwa wa michuano hiyo mara 11.

Lakini wakiwa hatari na wagumu kupoteza wanapocheza katika dimba la kimataifa la Cairo.

Kuelekea mchezo huo, Kocha Mkuu wa Simba, Abdelhak Benchikha, alisema mechi hiyo ni kubwa kwa timu zote mbili lakini anategemea kupata matokeo mazuri kwa sababu wachezaji wake wataingia kwa tahadhari kubwa ili kuhakikisha wanaondoka na furaha.

Benchikha alisema kuna tofauti kubwa alipocheza na Al Ahly akiwa na USM Alger na sasa anakutana na mpinzani huyo akiwa na Simba, ila anaweka wazi wamejiandaa vizuri kwa ajili ya kusaka ushindi.

"Matokeo ya nyuma ni mengine, timu iliyopo sasa ni tofauti na ya awali, Matokeo ya kesho (leo) ndio yataamua, kila mmoja anatambua ukubwa wa Al Ahly, siwezi kutabiri lakini tumejipanga kwa ajili kwa ajili ya kusaka ushindi.

Nilitamani kuwepo kwa wachezaji wote Zanzibar lakini hatukuweza kupata nafasi hiyo kwa sababu ya Kalenda ya FIFA Series, hali hiyo nimewaandaa vijana wangu kwa ajili ya kutafuta ushindi mbele ya Al Ahly," alisema Benchikha.

Kocha huyo aliongeza Simba imekuwa ikipata mabao mengi nyumbani lakini kwa mchezo wa leo anahitaji idadi kubwa pia ili mechi ya marudiano iwe nyepesi wanapokwenda ugenini.

"Matokeo ya michezo na Al Ahly ambayo aliyoyapata akiwa USM Alger yatamsaidia kwa timu aliopo sasa, kuiondoa Simba katika hatua ya robo fainali na kusonga mbele, kuchukuwa ubingwa mara 11 haituzui kumwondoa Al Ahly katika mashindano haya.

Nimezungumza na wachezaji wangu na wanahitaji hii mechi. Haiwezekani Simba kukosa matokeo hapa nyumbani, jambo ambalo ni gumu. Dhamana tulioipata kwa mashabiki wa Simba ni deni kubwa kwa benchi la ufundi na wachezaji, naomba wajitokeze uwanjani kwa wingi kwa sababu wanaenda kupigana hadi sekunde ya mwisho kutafuta matokeo tukiwa nyumbani na ugenini," alisema Benchikha.

Naye nahodha wa Simba, Shomari Kapombe, alisema wamejiandaa vizuri na wako tayari kupambana kutokana na maandalizi waliyoyapata na wanaimani ya kufanya vizuri katika mchezo huo.

Kapombe alisema wamejipanga kutumia vizuri uwanja wa Benjamin Mkapa kwa kuwapa furaha mashabiki wao.

"Tumepata muda mzuri wa kujiandaa na kukaa pamoja kama wachezaji, tunaimani kubwa ya kufanya vizuri, kikubwa Wanasimba wajitokeze kwa wingi uwanjani kuona timu yao inavyofanikiwa katika malengo yetu," alisema Kapombe.

Aliongeza anaenda kucheza robo fainali ya tano na malengo yao kama timu ni kutinga hatua ya nusu fainali na ili kufika huko watalazimika kupambana.

Kocha Mkuu wa Al Ahly, Marcel Koller, alisema haitakuwa mechi rahisi kwa sababu wanakutana na timu waliyokutana nayo kwenye robo fainali ya

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >